

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (wa pili kulia), Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Mkala (kulia), Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani, Zabron Yoti (kushoto), na Mwakilishi wa Ubalozi wa Marekani hapa nchini, Anathy Yagam, wakibonyeza kitufe kuzindua mpango wa Marekani wa upatikanaji wa chanjo ya Global Vax, katika viwanja vya Mwembe Yanga, Manispaa ya Temeke mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Lissu ampongeza Samia, atabiri ujio wa mabadiliko

**Na Salome Kitomari**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuanza mazungumzo na chama chake ni kielelezo tosha kwamba nchi inaelekea kwenye Katiba Mpya, mabadiliko makubwa ya kisheria, kitaasisi na muundo mzima wa utawala.

Akizungumza na Nipashe usiku wa kuamkia jana, Lissu alisema anashukuru kwa kulipwa haki yake ambayo ni mafao ya kazi ya ubunge aliyoifanya tangu Novemba 2015 hadi Juni 2019 ilipotangazwa bungeni kwamba amekosa sifa za kuwa mbunge.

Alisema licha ya mafanikio yanayoonekana sasa, bado kuna kazi kubwa ya kuondoa siasa zilizopita ambazo ziliacha majeraha kwa wengi, akiwamo yeye aliyepigwa risasi na watu wasiojulikana.

"Hiyo inahitaji Katiba Mpya, mabadiliko makubwa ya kisheria na kitaasisi na muundo mzima wa utawala. Kwa kuanza mazungumzo na CHADEMA, Rais Samia ameanza safari ya kuelekea kwenye mabadiliko hayo," alisisitiza Lissu ambaye amekuwa anaishi Ubelgiji tangu mwaka 2018 alipokwenda kwa matibabu.

Mwaka 2020, Lissu alirejea nchini kwa ajili ya uchaguzi mkuu ambao aliwania kiti cha Rais wa Tanzania, akitangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kushika nafasi ya pili nyuma ya Dk. John Magufuli (Hayati) aliyetangazwa mshindi.

**MADAI YA MATIBABU**

Kuhusu hali ya kisiasa, Lissu alisema kuna ahueni kubwa kulinganisha na wakati wa awamu ya tano, lakini bado kuna kazi kubwa ya kuondokana na kabisa na siasa zilizoumiza.

"Nimefurahi kwamba Rais Samia ameanza kurekebisha dhuluma niliyofanyiwa. Bado amebakisha madai yangu ya matibabu na kunihakikishia usalama wangu ili niweze kurudi nyumbani bila kuwa na hofu ya watu wasiojulikana. Natumaini na haya atayafanyia kazi," Lissu alisema.

Alifafanua: "Ni kweli nimeshalipwa kiinua mgongo changu, bado fedha za matibabu na hizo nimeambiwa niandike barua za kuzidai, na sasa ninakusanya nyaraka zote muhimu kwa kuwa nilitibiwa Nairobi na Ubelgiji."

Lissu, akiwa Mbunge wa Singida Mashariki na Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Septemba 7, 2017, majira ya saa nane mchana, alishambuliwa kwa risasi 32, kati yake 16 zikimpata mwilini, nje ya nyumba yake Area D, Site 3 jijini Dodoma.

Kiongozi huyo alijeruhuwa miguuni na tumboni wakati akiwa ndani ya gari lake aina ya Toyota Land Cruiser VX lililopata matundu 25 ya risasi upande alikokuwa ameketi.

Alipatiwa matibabu ya awali kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na baadaye Nairobi, Kenya kisha kuhamishiwa Ubelgiji ambako anaishi hadi sasa na ameshaweka wazi kwamba anaishi na risasi moja mwilini.

Siku chache baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Lissu alidai kutishiwa maisha na kulazimika kuondoka nchini Novemba 10, 2020, akitokea nyumbani kwa Balozi wa Ujerumani, akisindikizwa na Balozi wa nchini na maofisa wa Ubalozi wa Marekani nchini hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

Februari mwaka huu, Rais Samia akiwa kwenye ziara ya kikazi Ubelgiji, alikutana na Lissu kwa mazungumzo na baadaye mtaalamu huyo wa sheria alibainisha kuwa alimwomba Rais apate hati ya kusafiria ambayo aliipata ndani ya muda mfupi na alipwe stahiki zake.

Katika mazungumzo na Nipashe usiku wa kuamkia jana, Lissu alisema kuwa kabla ya kupatwa na madhila ya kupigwa risasi, alikuwa amekopa kwenye benki kadhaa, mojawapo ilimpeleka mahakamani kwa kuwa hakuwa amelipa mkopo wake kwa muda mrefu.

# Wabunge wataka uchunguzi hujuma Bwawa la Nyerere

**Na Romana Mallya,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Halima Mdee, ameitaka serikali kutoa maelezo kuhusu Sh. trilioni 6.5 ambazo analipwa mkandarasi anayejenga bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Julius Nyerere.

Amesema kuwa katika hilo, pia anahitaji kujua kiasi ambacho nchi inalipwa kutokana na uzembe alioufanya wa kuchelewesha kukamilisha mradi huo kwa mujibu wa mkataba.

Mdee aliyasema hayo jana bungeni jijini hapo alipochangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema anataka kujua nchi inapata nini kutokana na uzembe huo ili wajue kama bado kuna shida ya mikataba na wanasheria hawajajifunza kutokana na makosa.

"Katika mradi ambao serikali imewekeza kwa asilimia 100 ni Bwana la Mwalimu Nyerere, fedha za ndani za mradi huu ni Sh. trilioni 6.5, ulitakiwa kukamilika Juni 14, leo tunaambiwa umefikia asilimia 57.

"Tunajua kwenye mkataba kuna sura mbili, Mwanasheria Mkuu yupo hapa, upande mmoja ukiwa na uzembe upande mwingine lazima ufidiwe, ninakuomba waziri ukija kutujibu hapa utuambie hasara ambayo Tanzania imepata kwa mkandarasi huyu kutomaliza Juni 14 tunalipwa kiwango gani?" Alihoji.

Mbunge huyo alisema amesoma taarifa ya kamati ya sasa na ya mwezi Februari na kuona zinatofautiana.

"Mwezi wa pili Kamati ya Nishati na Madini imeeleza sababu tisa za msingi, hizo sababu tisa ni za uzembe wa mkandarasi, leo wanatuambia ni UVIKO-19 wakati Mheshimiwa Naibu Waziri ninakumbuka ulikuja katika Kamati ya Bajeti ukatuambia mkandarasi amesema UVIKO-19 lakini nyie kama serikali mmegundua tatizo siyo UVIKO-19 ila mkandarasi alikosea, alitakiwa ajenge matuta mawili lakini akajenga tuta moja wakati wa mafuriko ukavurugika," alisema.

"Haiwezekani kila siku tunapigwa, leo tunampa mtu kazi tena tunamlipa vizuri, kama kuna mtu analipwa kiroho safi ni huyu jamaa, hana hata stress (msongo wa mawazo), ninataka huyu anayekula fedha zetu bila msongo wa mawazo hajamaliza ujenzi kama mkataba unavyotaka, sababu zake alizotoa ni za uongo, waziri ulikuja hapa ukatuambia subiri mwezi wa sita si bado, mwezi wa sita ndio huu," alisema.

Mbunge huyo alimwomba waziri atoe majibu kuhusiana na suala hilo, akisema: "Kiroho safi, sina bifu na nyie, wote tunajenga nyumba moja, kiroho safi Sh. trilioni 6.5 ambazo tumempa huyu kwa heshima kubwa nchi inapata nini kutokana na uzembe? Ili tujue kumbe bado tuna shida ya mikataba, ili tujue wanasheria wetu bado hawajajifunza kutokana na makosa.

Mdee pia alihoji kuhusu mkataba ulioingiwa baina ya Shirika la Umeme (TANESCO) na Symbion ambayo sasa serikali inatakiwa kulipa Sh. bilioni 355 na kuhoji wanasheria walikuwa wapi.

Alimtaka waziri aeleze waliohusika wanawajibika kiasi gani na hatua zilizochukuliwa, akisema: "Baada ya kusema haya sina mengi sana, hayo mawili tu, nipate majibu kwa nia njema, nisipojibiwa tutakamata shilingi tu ili tujiachie zaidi."

Mbunge wa Tabora Kaskazini, Almas Maige, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumalizia Bwawa la Mwalimu Nyerere.

"Nina hofu ambayo sijui ninaogopa nini Kituo cha Msamvu kimeungua mara mbili ambacho ndicho kinalisha Bwawa la Nyerere, ninajiuliza ni hujuma au uzembe, wekeni kitengo cha uchunguzi ili kisiungue tena mara ya tatu," alisema.

Mbunge wa Lulindi, Issa Mchungahewa, alisema fedha zimewekwa kwenye mradi huo lakini hadi sasa haujakamilika ilhali ulitakiwa uwe umefika asilimia 98 ya ujenzi wake.

HABARI KITAIFA




Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea zawadi maalum kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama cha Makatibu Mahsusi Tanzania (TAPSEA), Zuhura Songambele Maganga, kabla ya kufungua mkutano mkuu wa kitaaluma kwa makatibu mahsusi, jijini Dodoma jana.
**PICHA: IKULU**

# Samia aonya 'masekretari' kuvujisha siri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameonya makatibu mahsusi na watunza kumbukumbu serikalini kuacha kupokea vijisenti na kuvujisha nyaraka za siri za serikali huku akisisitiza watakaobainika watachukuliwa hatua.

Akifungua jana Mkutano Mkuu wa Chama cha Makatibu Mahsusi Tanzania (TAPSEA), jijini hapo, Rais Samia alisema kuna wakati baadhi wakipelekewa vijisenti vidogo wanatoa nakala ya nyaraka za serikali na kumpa mtu kuzitumia vinginevyo.

"Unakuta nyaraka zipo kwenye mitandao wanazipata wapi kama sio nyie? Ni nyinyi na watunza kumbukumbu semeshaneni mnayo yafanya hayapendezi hata kidogo, unakuta taarifa za serikali zipo kwenye mtandao, barua kabisa Katibu Mkuu kasaini na ina muhuri huko ilikopokelewa imewekwa kwenye mtandao, ushahidi huo hapo, yawezekana watu wanasema ya kweli wanafichua majungu, au wanachomeana utambi, lakini ni nyaraka za serikali zipo kwenye mtandao inakuwaje," alisema.

Aliwaasa kuhakikisha siri za serikali zinakaa ndani kwa kuwa usalama wa serikali upo mikononi mwa makatibu hao na watunza kumbukumbu.

"Usalama wetu upo mikononi kwenu, kwahiyo mkiamua kusaliti ooho! Tutashikana huko mbele hatutakubali kusalitiwa lazima tufanye kazi kwa kushirikiana ili wote tufanye kazi kwa pamoja, wote twende pamoja," alisema.

Rais Samia aliwaasa uadilifu na kutunza siri za sehemu ya kazi na viongozi wao ni muhimu kwa kuwa wameaminiwa kwa kiasi kikubwa.

"Umeaminiwa kuwekwa pale kinachopita ni chako ni wewe na bosi wako hutakiwi kukisema kwa mtu mwingine, umeona la kufurahisha bana, subiri litokee mpongeze anayefurahishwa, umeona la kusikitisha bana, subiri litokee mpe pole, akikwambia kwanini hukunitonya mwambie sio kazi yangu, sasa ukitaka kujifanya mwema uonekane wewe ndio mtoa habari nzuri na wewe ndio muonea huduma watu hutafanya kazi yako vizuri," alisema.

Alibainisha kuwa alipokutana nao mwaka 2017 aliwaambia kuhusu siri za mdomo na kwamba wakiona kuna jambo linawakaba koo basi watafute ubuyu.

"Ukimaliza tema kokwa ndiyo utakuwa umetema lile lililokukaa kooni, huwezi kaa nalo nenda nalo nyumbani ukifika fungua flash (msalani) sema humo ndani kisha piga flash yaende na maji moyo wako utakuwa umesuuzika, si huwezi kukaa bila kusema, lakini sio kutafuta mtu na kumhadithia, hata mahusband (waume) wetu unakwenda kumhadithia kwa mahaba tu ukiamini atatunza siri kumbe naye ana mtu wa kumhadithia," alitahadharisha.

Kuhusu siri za viongozi wao alisema; "Sio wewe tena umeona bosi kaingiza king'asti hapo kwanza unakitizama kwa jicho la kushoto pembeni halafu ukitoka mh leo...mh au umeona kisiri cha mtu kimepita anapewa adhabu, mwezangu nikwambie kaa vizuri mambo yanakuja hiyo itakuwa sio uadilifu."

"Ungekuwa siri za mahali pako pa kazi unazitoa mambo yanajulikana tu wakina nani hao wa mitandao wanazitoa tu bosi asingeupiga mwingi, lakini inawezekana kwasababu wewe unafanya wajibu wako kwa hiyo mtambue kwamba umahsusi wenu upo hapo unapofanya wewe vizuri na mimi nitafanya vizuri, lakini ukiniharibia basi tunaharibika sote," alisema.

Aliongeza "Katibu Mahsusi lazima awe mweledi na mwadilifu, unapokosa uadilifu umejitoa kwenye ile sifa ya ukatibu mahsusi wewe unakuwa ni mpiga chapa tu na unapokosa weledi ni vile vile unakuwa mpigachapa na sio katibu mahsusi, mmepewa jina mahsusi kwa kazi maalum mnazozifanya."

Kuhusu bajeti ya mafunzo, kuhudhuria mikutano na kujiendeleza kielimu, Rais Samia alisema lazima viongozi watenge bajeti huku akimwagiza Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, Jenista Mhagama, kuangalia suala la kupandisha madaraja kwa makatibu hao na fedha kama zimelipwa.

"Na sasa hivi kama muundo umekamilika niwaelekeze kasimamieni muundo na mhakikishe wanapanda madaraja yao na kama kuna madai yanalipwa ipasavyo," alisema.

Alitaka kupitia Chuo cha Utumishi Tabora sasa wazalishwe, wawalee na kuwakuza kimaadili ili kuwapanga kufanya kazi na viongozi.

"Inawezekana hapo katikati mtu ana mvuto mzuri, ana kicheti chake ndio bosi anamwajiri huyu ndio Katibu wangu Mahsusi, mtu akiingia hapo akute kuna kitu, lakini pengine kazi maadili hakuna kwa hiyo turudi kwenye maadili ya kazi zao.

Kwa hiyo nimetoa agizo la chuo kizalishe na wanaozalishwa wajengwe kimaadili, wapate mafunzo halafu wasambazwe kwenye ofisi kufanya kazi," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar, Mhandisi Zena Said, aliwataka waajiri wote nchini kutoa nafasi kwa makatibu mahsusi kuhudhuria mikutano hiyo.

Kadhalika, Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema muundo wa utumishi wa umma wa kada ya Makatibu Mahsusi utaanza kutekelezwa mwaka wa fedha wa 2022/23, huku Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, akiagiza Wakurugenzi wa Mamlaka za Mitaa na watendaji wa wizara hiyo kutowazuia makatibu mahsusi kushiriki shughuli za TAPSEA.

Awali, Mwenyekiti wa TAPSEA, Zuhura Maganga, alimpongeza Rais Samia kwa uamuzi wake wa kuongeza mishahara na kuainisha kero wanazokabiliana nazo ikiwamo waajiri kutopanga bajeti za mafunzo kwa watumishi wa kada hiyo.

# Mafuta bei 'chee' yaibua tabasamu kwa madereva

**Na Salome Kitomari**

WASOMI, wasafirishaji na wananchi wamepongeza hatua ya awali ya serikali kuweka Sh. bilioni 100, kwenye mafuta ambayo imesaidia unafuu kushuka bei ya bidhaa hiyo.

Aidha, wamesema wanasubiri kwa hamu kubwa Juni 16, mwaka huu, siku itakaposomwa bajeti ya nchi ili kuona kodi zitakazoondolewa zitakavyosaidia kushusha bei ya bidhaa hiyo muhimu kwa uchumi wa nchi.

Mei mwaka huu, Rais Samia alikutana na Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba na Waziri wa Nishati, January Makamba, na viongozi wengine akaelekeza kutolewa kwa fedha hizo kupunguza makali, huku hatua zaidi za kikodi kujulikana Juni 16, mwaka huu.

Juni mosi, mwaka huu, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilitangaza bei kikomo kuwa ni lita moja ya petrol inauzwa Sh. 2,994 diesel Sh. 3,131.

Msemaji wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Mustapha Mwalongo, alisema hatua za sasa ni nzuri zimetoa unafuu wa bei ya bidhaa hiyo, na kwamba wanasubiri hatua za kikodi ambazo zitapunguza zaidi.

"Tunaipongeza serikali, tunamshukuru Rais Samia kwa kusikiliza kilio chetu, ila serikali ifanye kila linalowezekana kushusha zaidi, hali ya uchumi sio kwa wasafiri tu bali watumiaji wa usafiri," alisema.

"Wakishusha mafuta kutakuwa na unafuu mkubwa sana, kuna bei elekezi, lakini biashara yetu ni ya kukubaliana maana kuna wakati unakwenda kwa bei ya chini sana wakati mafuta yako juu," alisema.

Aidha, Mwalongo alisema ni muhimu serikali iongeze juhudi yafike Sh. 2,000 na anaamini serikali sikivu ya awamu ya sita itaongeza kupata unafuu.

"TABOA tunasubiri kwa hamu kwamba bajeti kuu inaweza kuondoa kodi nyingi inawezekana itasaidia kama alivyotoa ushauri Rais," alisema Msemaji huyo.

Mhadhiri wa Uchumi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Razack Lokina, alisema jitihada za serikali ni nzuri ingawa zinasubiriwa za bajeti ya serikali.

Alisema mafuta yakipanda yanachangia mfumuko wa bei, hatua ya serikali ilikuwa ni sawa, bila hivyo yangeendelea kuwa juu zaidi, gharama ya maisha ingekuwa kubwa licha ya mishahara kuwa bado haijaongezeka.

"Itasaidia kupunguza ukali wa maisha kutokana na bei ya vitu sokoni, inagusa maisha ya mtu, fedha yake ndogo inatumika kununua vitu ambavyo havitoshelezi mahitaji yake," alisema msomi huyo.

Mwenyekiti wa waendesha Bajaj wenye ulemavu Dar es Salaam, Paul Masamaki, aliishukuru serikali kwa hatua ilizochukua kwa sasa na kuomba iendelee kuwasaidia wananchi, na kwamba kwa nchi za Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo ina bei nafuu ya mafuta, na kwamba kodi zikiondolewa mwananchi wa chini ataona faida.

Alisema kwa sasa serikali imeweka ruzuku lakini bado ni ndogo kwa kuwa bei za nauli na bidhaa haziwezi kushuka lakini kukiwa na punguzo kubwa zitashuka.

# Ajinyonga madai ya kujifungua mtoto mwenye kichwa kikubwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKAZI wa Kijiji cha Kanikelele, wilayani Njombe, Sara Lukelema (24), amefariki dunia kwa kujinyonga na kamba chumbani kwake huku sababu ikitajwa kuwa kujifungua mtoto mwenye kichwa kikubwa na mgongo wazi.

Akizugumza na Nipashe nyumbani kwake, mama mzazi wa marehemu, Constanzia Msambwa, alisema siku ya tukio alimuaga mwanawe kuwa anakwenda shambani.

"Ilikua Jumatatu ya Mei 23, nilimuaga asubuhi kuwa nakwenda shambani na yeye kubaki nyumbani, lakini majira saa 11 jioni wakati natoka shamba nikakutana na wanangu wengine njiani nikawaambia tangulieni nyumbani," alisema.

Muda mchache aliwaona wanarudi wakikimbia huku wakisema mama mbona dada tunamuita haitiki? "Nikasema haitiki amefanyaje, wakasema sijui mbona mlango umefungwa haufunguki na mtoto analia ndani, mwingine akasema mbona ana kamba, kwahiyo nikaongozana na kiongozi wa kitongoji ili kujua tatizo," anasimulia mama huyo.

Alisema pamoja na kujifungua mtoto mwenye tatizo, ugumu wa maisha umesababisha kwa sababu ya kuhitaji matibabu zaidi.

"Sijui alikuwa na mawazo ya mtoto yule mwenye ulemavu wala sijaelewa vizuri," alisema.

Awali, alisema walianza kufuatilia suala la matibabu kwa ajili ya mtoto huyo Hospitali ya Lupembe baadaye wakahamishiwa Hospitali ya Mji Njombe Kibena.

"Baada kufika Kibena walisema anatakiwa kufanyiwa operesheni kwa sababu hadi miguu ilikuwa na ulemavu na hivyo tukaenda hospitali ya rufaa nako wakasema hawawezi na badala yake tumpeleke rufaa Mkoa wa Mbeya."

Walipofika Mbeya, walitakiwa kulipa Sh. 650,000 kwa ajili ya matibabu na alipopiga simu kijijini kuomba msaada ndugu zake walikopa na mtoto alifanyiwa upasuaji wa mgongo wazi na baadaye kurudi nyumbani.

"Baadaye tukampeleka kutoa nyuzi, daktari aliyemtoa nyuzi hapa Kanikelele alishauri nirudi tena rufaa, lakini uwezo sina hadi leo hii, kwahiyo mwanangu anavyomuangalia mtoto anaona miguu haitikisiki kama alikata tamaa," alisema Costanzia.

Kilichokuwa kinawapa changamoto alisema ni namna ya kumlea mtoto huyo kutokana na kuhitaji kufanyiwa matibabu zaidi.

Mmoja wa majirani, Agnes Joseph, alisema uamuzi aliochukua mwanamke huyo ni mgumu wa kumuachia jukumu la malezi mama yake bila ya msaada.

"Huyu mtoto ni mlemavu sawa, asingevunjika moyo badala yake angeshirikiana na mama yake katika malezi na sio kumuachia peke yake maana hata huko shamba hatoweza kwenda tena," alisema Agnes.

Naye Mwenyekiti wa kitongoji Luganga, Roma Mhiche, alisema kama kitongoji wanafanya michango mbalimbali kumsaidia mtoto huyo kupata mahitaji ikiwamo maziwa kwa sababu hakuwahi kunyonya maziwa ya mama yake tangu kuzaliwa.

"Tunachangishana michango mbalimbali ili kuweza kumnunulia mtoto maziwa ya ng'ombe hivyo tunaomba wadau na serikali pamoja na wakazi wa maeneo haya kusaidia hii familia isiwe katika msongo wa mawazo," alisema Mhiche.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Njombe, Hamis Issah, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo kuwa mwanamke huyo alijinyonga nyumbani kwao kutokana na kujifungua mtoto mwenye kasoro.

"Huyu mama amejifungua mtoto, lakini ana kasoro ya kuwa na kichwa kikubwa na mgongo wazi na mama akachukua maamuzi ya kujinyonga," alisema Kamanda Issah.

Kamanda Issah alitoa wito kwa wakazi wa Mkoa wa Njombe kuacha kufanya matendo ya ukatili kwa kuwa vitendo hivyo vimeendelea kukithiri mkoani humo.



Mkurugenzi Mtendaji Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akipokea tuzo ya Mwanabenki Bora wa Mwaka kwa wateja wadogo kwa Mkuu wa Wakala wa Wateja na Usambazaji wa Benki ya CRDB, Ericky Willy, aliyeipokea kwa niaba yake wakati wa Mkutano wa Benki Afrika 4.0, uliofanyika jijini Nairobi hivi karibuni. Waandaaji wa mkutano huo walishukuru mchango wa Nsekela katika maendeleo ya sekta ndogo ya rejareja nchini Tanzania na dhamira ya benki hiyo katika ushirikishwaji wa kifedha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Familia yagoma kuzika ikitaka ripoti ya polisi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

FAMILIA ya Kibabu Msese (26), mkazi wa Wilaya ya Karatu mkoani Arusha aliyefariki katika mazingira ya kutatanisha baada ya kukamatwa na polisi wilayani humo, imesema haitauzika mwili huo hadi hapo itakapopata majibu ya kilichosababisha kifo cha ndugu yao.

Akizungumza kwa uchungu nyumbani kwa marehemu, kaka wa marehemu, Petro Msese, alisema jana kuwa wanaiomba serikali kuhakikisha haki inatendeka dhidi ya ndugu yao huyo aliyedai kauawa kutokana na kipigo cha askari polisi baada ya kukamatwa.

"Sisi familia tumekubaliana hatutazika mwili wa ndugu yetu mpaka tutakapopata majibu ya kina juu ya kilichosababisha kifo chake, kwa sababu mwili unaonekana ameng'olewa kucha za miguu lakini pia amevunjwa shingo," alidai.

Mke wa marehemu, Catherine Jeremia, alisema siku ya tukio mtoto wao mdogo alikuwa mgonjwa ndipo mumewe akamwambia anakwenda kuchukua pikipiki ili wampeleke hospitalini lakini ghafla alishangaa kumwona mume wake amerudi akiwa ndani ya gari la polisi.

Alidai kuwa baada ya kuona gari la polisi, alipigwa na butwaa na kuuliza 'kuna tatizo gani?' na kujibiwa na mmoja wa askari hao waliokuwa na silaha kwamba asiwe na wasiwasi, angejua kilichowapeleka polisi huko nyumbani kwake.

"Walifanya ukaguzi kila mahali ndani ya nyumba, hawakupata chochote. Wakakagua kwa kupanda juu ya dari la nyumba ambapo hawakupata kitu kisha wakakagua chooni na jikoni bila kupata chochote," alisimulia.

Mjane huyo alidai kuwa baada ya kukosa vitu walivyovitaka, askari polisi hao waliketi sebuleni kisha wakadai stakabadhi ya simu yake ya kiganjani na 'sabufa' na kwamba mumewe aliwapatia na baadaye waliamua kuchukua kiambaza (screen) na kuondoka nacho.

Mjane huyo aliyesimulia mkasa huo huku mara kadhaa akikatishwa na hisia za msiba na kuhamia kwenye kilio, alidai aliandaa chakula na kukipeleka Kituo cha Polisi Karatu lakini mumewe aliyekuwa mahabusu huko alipoitwa hakuitika, na kwamba askari polisi aliyekuwa zamu alimtaka mjane huyo aondoke kwa madai kuwa angemwona mumewe siku iliyokuwa inafuata.

"Nilifika nyumbani nikamweleza shemeji yangu kuwa sikufanikiwa kumwona mume wangu ili apewe chakula lakini aliniambia atakwenda mwenyewe siku itayofuata na alipofika kituoni, aliambiwa kuwa ndugu yake aliugua ghafla na kupelekwa hospitalini hapa hapa Karatu," alidai.

Alisema baada ya kufika hospitali waliambiwa kuwa ndugu yao alikuwa amepelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru) baada ya hali yake kuwa mbaya na walipokwenda hospitalini, walikuta ameshafariki dunia.

"Ninaomba serikali inisaidie haki ya marehemu mume wangu ipatikane kwa sababu kifo chake kina utata mkubwa na ameniacha na watoto wawili ambao bado walikuwa wanahitaji malezi bora ya baba yao," alisema.

**KAULI YA POLISI**

Hata hivyo, akizungumza jana jijini Arusha na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo alidai mtuhumiwa huyo alifariki dunia Mei 31, mwaka huu kwenye hospitali hiyo na kwamba alikuwa jambazi.

# Mwanafunzi anajisiwa, anyongwa hadi kufa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamsaka mtuhumiwa wa mauaji ya mwanafunzi wa darasa la pili mwenye umri wa miaka saba ambaye alinajisiwa na kunyongwa hadi kupoteza maisha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake alisema, mtuhumiwa huyo anadaiwa kumnajisi mtoto huyo na baadaye kumnyonga kwa kutumia chandarua.

Alisema tukio hilo lilitokea juzi nyumbani kwa mtuhumiwa huyo katika Kitongoji cha Vitendo Misugusugu na wanaendelea kumsaka.

Kamanda Lutumo alisema uchunguzi wa awali umebaini mtuhumiwa huyo alifanya tukio la mauaji akiwa anamnajisi mtoto huyo kwa kumfumba mdomo ili asipige kelele.

Alitoa wito kwa wazazi kuwafuatilia watoto wao na kuzungumza nao mara kwa mara kujilinda wenyewe kwa wenyewe. Ofisa Habari na Mawasiliano wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani (Tumbi), Saimon Lymo, alikiri kupokewa kwa mwili wa mwanafunzi huyo ukiwa na sare za shule na ulifanyiwa uchunguzi na kukabidhiwa kwa ndugu.

Akizungumzia tukio hilo, mama mzazi wa mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa), alisema mtoto wake kwa utaratibu wa kila siku huingia darasani saa nne asubuhi na siku ya tukio alikuwa akitoka nyumbani kwenda shule.

Alisema siku ya tukio aliporejea nyumbani kutoka kwenye shughuli zake hakumkuta mwanawe ndipo alipoanza kufuatilia kwa wanafunzi ambao mara kwa mara anaongozana nao.

Mama huyo alisema alifika kwa rafiki wa mwanawe ambaye mara nyingi anaongoza naye kwenda shule na kuambiwa kuwa mwanawe hakuonekana shuleni aliishia njiani.

Rafiki wa mwanafunzi huyo alisema wakiwa njiani rafiki yake alimwambia amsubiri akaombe miwa kwa mtu ambaye wamezoea kumuita mjomba.

Hata hivyo, alisema baada ya kwenda alichukua muda mrefu kutoka na alipojaribu kumuita kwa muda ili waondoke, hakuitika. Alisema baada ya kuita kwa muda alitokea kaka huyo wanayemuita mjomba ambaye alikuwa akijaribu kumsogelea na kumpa hofu jambo lililomfanya akimbie kwenda shule.

Baada ya kupata maelezo akiwa na baadhi ya majirani na viongozi wa ubalozi kwenye mtaa wake, walienda hadi nyumbani kwa mtuhumiwa na kukuta mlango umeegeshwa.

Walifungua na kuingia ndani, lakini hawakukuta mtu, katika ukaguzi kwenye moja ya vyumba walikuta mwili wa mtoto huyo ukiwa umeshafariki na umefungwa na mashuka.

Alisema walitoa taarifa polisi na walifika kuchukua mwili huo kuupeleka hospitali kwa ajili ya uchunguzi na baadaye kuwakabidhi kwa ajili ya maziko.

Baadhi ya majirani walisema mtuhumiwa ni mkazi wa eneo hilo kwa miaka miwili akiishi katika nyumba hiyo kama mwangalizi na baada ya kufanya tukio hilo alitoroka kusikojulikana.

## Wataka elimu tasnia ya habari iheshimiwe

Na Mary Geofrey

WAANDISHI wa habari nchini, wametoa mapendekezo, kuhusu kiwango cha elimu kutiliwa mkazo katika mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya habari nchini.

Mapendekezo hayo waliyatoa jana, wakati wa mkutano wa waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari kwa njia ya mtandao, ulioandaliwa na Jukwaa la Wahariri nchini (TEF), kwa lengo la kujadili kuhusu mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya habari yaliyowasilishwa serikalini.

Mwandishi wa Habari wa Televisheni ya ITV, Godfrey Monyo, alisema suala la kiwango cha elimu ni la kuzingatia ili kupandisha hadhi ya tasnia ya habari.

"Sekta nyingine zina viwango vya elimu na vinajulikana, badala ya wote kuonekana kuwa hatuna maana ndani ya jamii kwa sababu ya watu wachache, naomba suala la elimu litiliwe mkazo wa hali ya juu," alisema Monyo.

Naye Dk. Tumaini Msowoya kutoka gazeti la Mwananchi mkoani Iringa, alisema suala la elimu ni muhimu ili kufanya kazi kwa weledi mkubwa hasa ikizingatiwa kuwa, wanahudumia jamii.

"Ni muhimu hili suala la kiwango cha elimu lizingatiwe ili tuwe na wanataaluma ambao wanazingatia maadili ya uandishi wa habari na kuhudumia vyema jamii inayowategemea," alisisitiza.

Naye mwandishi wa habari kutoka Radio One, Christopher James, alisisiza kuhusu umuhimu wa wanahabari kuwapo kwa sheria inayowabana wasio na taaluma kuingilia faini hiyo kama ilivyo sasa kwa wasanii na waburudishaji kutangaza.

"Sheria itamke wazi, hili suala la watu mashuhuri kuingilia fani na kuanza kutangaza moja moja kwenye vituo vya redio au runinga sio sawa, linashusha hadhi ya taaluma hii," alisema.

Naye Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alitaka kuwapo na mjadala wa kitaifa ili kupata suluhu ya moja kwa moja kuhusu sifa za kuwa mwandishi wa habari.

Alisema wameanzisha ushirikiano na wadau wengine wa habari likiwamo Baraza la Habari nchini (MCT) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) kwa ajili ya kuwasilisha maoni yao kuhusu marekebisho ya mabadiliko hayo ya sheria badala ya kila taasisi kutoa maoni yake.

"Kabla hatujakutana na Rais Samia Suluhu Hassan, Julai mwaka huu, kwanza tutakutana na Waziri wa Habari na Teknolojia ya Mawasiliano, Nape Nnauye ili kujadili kwa kina," alisema Balile.



Balozi wa Tanzania nchini Uganda, Dk. Azizi Mlima (kushoto), akisalimiana na mmoja wa askari, alipotembelea kikundi maalum cha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vitakavyoshiriki zoezi la ushirikiano imara Afrika Mashariki nchini humo. **PICHA: HISANI YA JWTZ**

# Katibu Mkuu wa CCM amtaka mbunge kuwezesha wananchi

Na Maulid Mmbaga

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amemtaka Mbunge wa Itilima, Njalu Silanga, kuwawezesha wakulima wa eneo hilo na kuhakikisha kila tarafa inapata mashine ya kukamua mafuta ya alizeti ili kuongeza thamani ya zao hilo.

Chongolo alitoa agizo hilo jana alipowasili wilayani Itilima mkoani Simiyu, wakati akiendelea na ziara yake yenye lengo la kuhamasisha uhai wa chama ngazi za mashina na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Najua mbunge wenu ana wajibu wa kuwasaidia mashine za kuchuja mafuta ya alizeti, wasaidie wananchi hawa wapate mashine za kuchuja mafuta ya alizeti angalau kwa mashine moja kwa kila tarafa na hili litawasaidia sana kuongeza thamani ya zao hili," alisema Chongolo.

Aliongeza kuwa kitendo cha kufunga mashine, wakulima wataanza kuuza mafuta badala ya alizeti ghafi, kwa sasa mafuta ya alizeti ndiyo bora na ghali zaidi, ambayo yatawezesha wananchi kupata fedha za kutosha.

Vile vile, alimtaka mkuu wa mkoa huo kufuatilia na kuhakikisha wakulima ndani ya mkoa huo wanapatiwa mbegu nzuri na ya bure ili kuongeza tija ya wakulima wa alizeti.

Katika wilaya hiyo Chongolo alipokea changamoto ya uhaba wa watoa huduma ya afya, alisema serikali imetoa ajira nyingi kwa watoa huduma ya afya lengo likiwa ni kupata madaktari wa kutosha katika vituo vya afya.

"Hata hapa mkishapata majengo kwa ajili ya kituo cha afya wahudumu waanze kufika mapema kutoa huduma ya mama na mtoto, kuwapoteza hao ni hasara kubwa kwa nchi yetu, tuwalinde," alisisitiza Chongolo.

Mbunge wa Jimbo la Itilima, alibainisha changamoto zinazowakabili katika eneo hilo ikiwamo ukosefu wa sehemu ya dawa wakati wameshapeleka zaidi ya Shilingi bilioni moja Bohari ya Dawa (MSD).

Alisema pamoja na Halmashauri ya Itilima kupeleka fedha za dawa, hadi sasa hawajazipeleka wilayani hapo jambo ambalo linasababisha changamoto ya matibabu kwa wananchi wa eneo hilo.

"Tuna bilioni moja na kitu tumepeleka MSD, lakini vile vifaa tiba bado havijafika katika halmashauri yetu ya Wilaya ya Itilima, ni fedha nyingi tumependekeza, lakini bado wananchi hawajapata huduma inayostahili," alisema Silanga.

Katika mafanikio alibainisha kuwa wamekusanya Sh. bilioni 1.2, huku akishukuru serikali kwa kuwasaidia wananchi wa eneo hilo kupeleka mamilioni kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maendeleo ikiwamo shule, barabara, vituo vya afya na mradi wa maji.

# ACT yataka hatua za dharura Kigamboni

Na Mwandishi Wetu

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kuchukua hatua za dharura kuwanusuru wananchi wa Kigamboni dhidi ya adha ya usafiri kutoka Kigambani kuelekea maeneo mengine ya Dar es Salaam.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, wakati wa Mkutano Mkuu wa ACT-Wazalendo Jimbo la Kigamboni uliofanyika Kata ya Kigamboni.

"Ili mwananchi wa Kigamboni aweze kwenda mjini, ni lazima apitie Daraja la Kigamboni (Daraja la Nyerere) au Kivukoni. Kwa upande wa darajani, ni lazima kulipia magari.

"ACT-Wazalendo tunasema tunajua daraja hili lilijengwa kwa ubia na NSSF. Hoja yetu ni kuwa tozo ya kuvuka darajani iondoshwe, kilichokusanywa kinatosha. Sehemu ya mkopo iliyobaki ilipwe na serikali. Hatua ya serikali ya hivi karibuni haitoshi, tozo zifutwe kabisa," alisema.

Kuhusu kivuko, Ado alidai ni dhahiri kuwa mamlaka husika imeshindwa kuendesha vivuko vya Kigamboni kwa kuwa hakuna ukarabati wa vivuko wa mara kwa mara na wananchi wanalazimika kutumia muda mwingi kwa sababu vivuko vya Mv. Magogoni, Mv. Kigamboni na Mv. Kazi huharibika mara kwa mara.

"Mamlaka husika iwajibike juu ya hili. Hata CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) ametaja ubadhirifu mkubwa wa mafuta kwenye vivuko. Ni lazima menejimenti ya vivuko iwajibishwe au viwekwe chini ya msimamizi mwingine," alishauri.

Ado pia alisema chama chao kupitia kamati ya wasemaji wa kisekta itaendelea kupaza sauti dhidi ya madhila na kero zinazowakabili wananchi wa Kigamboni na Watanzania kwa ujumla.

**KIVUKO CHAHARIBIKA**

Katika hatua nyingine, Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) jana ulitoa taarifa kwa umma kuhusu kuharibika kwa Kivuko cha MV. Magogoni kinachotoa huduma kati ya Magogoni na Kigamboni.

Wakala huo kupitia kitengo cha masoko na uhusiano, ulibainisha katika taarifa yake hiyo kuwa kivuko hicho kilishindwa kutoa huduma jana asubuhi kutokana na kupata hitilafu kwenye mifumo ya uendeshaji wa kivuko hicho na hivyo kusababisha huduma kusimama kwa muda.

"Mafundi wetu wanaendelea kurekebisha mifumo ya mitambo ya uendeshaji iliyoathirika ili kurudisha huduma za kivuko haraka iwezekanavyo.

"Shughuli za uvushaji abiria zinaendelea kwa kutumia kivuko cha MV. Kigamboni. TEMESA inawaomba radhi abiria wote wanaotumia kivuko cha Magogoni-Kigamboni kwa usumbufu uliojitokeza na inawashauri watumie njia mbadala ya Daraja la Nyerere ili kuepusha usumbufu," wakala huo ulifanua katika taarifa hiyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo alilotoa Rais Samia kuhusu TASAF liheshimiwe

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi alikabidhi magari 123 kwa wakurugenzi wa halmashauri nchini kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini nchini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Katika hafla hiyo iliyofanyika Viwanja vya Posta, Kijitonyama, Dar es Salaam, Rais alizungumza mambo mbalimbali ikiwamo kuagiza viongozi wa kisiasa katika ngazi za chini kujumuishwa katika kundi la wanufaika wa mpango huo.

Pamoja na hilo, Rais aliagiza viongozi na watendaji wa TASAF kujikita zaidi katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya rasilimali zao badala ya kuwapatia fedha pekee. Kwa kufanya hivyo, alisema itasaidia kuwaondoa watu hao katika umaskini unaowakabili na wakati huo huo, kutekelezwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG).

Bila kuruka maneno, Rais alisema mtu kuwa katika nafasi ya kisiasa haimaanishi kuwa ana maisha mazuri kwa kuwa wako baadhi ambao wanaishi maisha duni. Hatua ya baadhi ya viongozi kuwa na vyeo, imekuwa ikiwanyima fursa mbalimbali licha ya kwamba miongoni mwao wanaishi maisha duni.

Kama alivyosema Rais Samia, viongozi wanapochaguliwa katika nafasi, kigezo cha kuwa na maisha bora hakipo bali huangaliwa uadilifu, uwezo wao katika kuongoza, heshima na busara walizo nazo katika jamii wanazoishi. Hii ni kutokana na miiko ya uongozi iliyowekwa na waasisi wa taifa kutokana na siasa ya Ujamaa na Kujitegemea iliyokuwapo baada ya kupata uhuru.

Pamoja na ukweli huo, kumekuwa na kasumba kudhani kwamba mtu anapochaguliwa kushika nafasi fulani, anajimudu kimaisha licha ya ukweli kwamba wako ambao hata uwezo wa kuhimili milo mitatu kwa siku hawana. Hatua hiyo ya kutokupata fursa kama zinazopatikana kupitia TASAF zimekuwa zikiwapa kisogo na matokeo yake kuendelea kuishi katika umaskini uliokithiri. Kwa maneno mengine, kunyimwa kwao fursa hizo ni moja ya aina za ubaguzi katika jamii. Mfano halisi ni viongozi walioko katika vyama vya siasa kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji hadi kata ambao baadhi yao maisha yao ya kila siku ni ya kijungujiko yao.

Kuhusu elimu, ni jambo la msingi kutokana na uhalisia wa maisha ya Watanzania wengi kutokuwa na uelewa juu ya masuala mbalimbali ikiwamo kutumia rasilimali walizo nazo au zinazowazunguka katika kujiletea maendeleo.

Katika jamii za wafugaji, kwa mfano, ni jambo la kawaida kumkuta mtu akiwa na ng'ombe wengi, lakini anaishi maisha duni. Kwa maana hiyo anakuwa mtumwa wa mifugo badala ya kuwa mnufaika au anakuwa mchungaji na si mfugaji.

Agizo la Rais juu ya viongozi wa kisiasa kunufaika na fursa mbalimbali hasa zile za TASAF, limetolewa kwa wakati mwafaka na linastahili kupongezwa kwa kuwa ameonyesha upendo wa hali ya juu kwa wananchi wake.

Pia umefika wakati kwa Watanzania kuondokana na ufugaji au ukulima wa mazoea ambao umezidi kudumisha umaskini siku hadi siku badala ya kujikwamua na shughuli husika.

Ili kufanikiwa katika hilo, elimu inapaswa kutolewa kwa kiwango cha hali ya juu ili wananchi walime na kufuga kwa njia za kisasa. Yote hayo yatafanikiwa iwapo watendaji watakwenda kwa wakulima na wafugaji badala ya kukaa kwenye ofisi.


Kwa mantiki hiyo, kinachofuata sasa ni utekelezaji ikiwamo kuwabaini wale wasio na uwezo na hatimaye kupatiwa misaada. Tunaamini kwamba kwa kuwa ni viongozi katika jamii, pia watatoa ushauri mzuri namna ya wananchi kuboresha maisha yao kupitia uwezeshwaji kutoka TASAF.

Pamoja na pongezi hizo, suala la mhusika anatoka chama gani cha siasa lisijitokeze kwani kuna uwezekano katika maeneo likajitokeza jambo hilo na hatimaye kuibuka kwa ubaguzi kwa misingi ya kisiasa.

Ni vyema kwamba jambo kama hilo litakapojitokeza, likemewe mara moja na wahusika wachukuliwe hatua stahili. Tunasema hivyo kwa sababu Watanzania ni wamoja bila kujali imani zao za kidini, rangi, siasa wala kabila.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Pongezi serikali kushusha mafuta, lakini nauli zetu nazo zifikiriwe

Na Adam Fungamwango

**HATIMAYE** serikali imesikia kilio cha Watanzania kwa kushuka bei ya mafuta ya petroli na dizeli kuanzia juzi.

Hayo ni matokeo ya serikali kutoa ruzuku kukabili ongezeko la mafuta hayo hivi karibuni.

Mwezi uliopita Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alitangaza uamuzi huo baada ya kuwepo kilio cha wananchi kupanda kwa gharama za maisha, na hasa baada ya bei ya mafuta kupanda.

Akatoa kiasi cha Sh. Bilioni 100 kusaidia kupunguza maumivu ya kupanda kwa gharama za maisha kutokana na hilo.

Tayari utelezaji wake umeanza kwani juzi, Mkurugenzi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Modestus Lumato alisema pamoja na kwamba bei ya mafuta kwenye soko la dunia imeendelea kupanda zaidi na hasa kutokana na vita inayoendelea kati ya Russia na Ukraine, lakini serikali, chini ya Rais Samia ipo kwa ajili ya kuhudumia Watanzania na imesimamia ahadi yake iliyoweka, nia ni kuleta unafuu kwenye maisha ya wananchi wote.

Mkurugenzi huyo akatangaza kupungua kwa bei hiyo kwa viwango tofauti kutokana na mikoa husika.

Hii inaonyesha kuwa tayari serikali imeshafanya kazi yake kama ilivyoyowaahidi Watanzania.

Tunaipongeza serikali kwa hiki ambacho imekifanya, si kwa kujali wananchi na maisha yao kwa ujumla, lakini pia kutekeleza kile ambacho imekiahidi.

Na si kukitekeleza tu, lakini kukitekeleza kwa wakati muafaka. Hii inaonyesha kuwa serikali imekuwa ikisikia vilio vya wananchi wake na kuvifanyia kazi kwa haraka na kwa muda husika.

Kama ambavyo serikali imesikia vilio vya wananchi na kuchukua hatua kwa haraka, tena ikiingia gharama, ni wakati sasa kwa wafanyabiashara na wasafirishaji nao kuiiga serikali kwa kile ilichokifanya.

Nao wanapaswa kusikia vilio vya wananchi na kupunguza bei ya bidhaa na nauli, ili kwenda sambamba na kile ambacho serikali ilichokuwa ikikusudia.

> **Serikali haikuwa inakusudia kutoa ruzuku kwa ajili ya kuwanufaisha au kuwapa unafuu wafanyabiashara na wasafirishaji ili wapate faida kubwa kwenye mabasi au bidhaa zao, badala yake ilikuwa inalenga kuwapunguzia mzigo wa gharama wananchi wake.**

Serikali haikuwa inakusudia kutoa ruzuku kwa ajili ya kuwanufaisha au kuwapa unafuu wafanyabiashara na wasafirishaji ili wapate faida kubwa kwenye mabasi au bidhaa zao, badala yake ilikuwa inalenga kuwapunguzia mzigo wa gharama wananchi wake.

Ili kwenda sambamba na mawazo ya serikali, wafanyabiashara na wasafirishaji wanatakiwa kuangalia sasa namna ya kupunguza bei ya bidhaa na nauli ambazo tayari zimeshapanda.

Sitarajii kuwa watakuwa wazito kufanya hivyo, wakati serikali imefanya wepesi, tena ikiingia gharama kubwa ya kutoa ruzuku.

Kwa sasa bei za bidhaa zimekuwa zikipanda mara dufu kwa sababu mbalimbali, lakini pia wafanyabiashara wamekuwa wakifanya hivyo kwa ajili ya kutaka kujipatia faida kubwa kwa kisingizio cha vita inayoendelea.

Kwa sasa serikali imeamua kukata mzizi wa fitina, sidhani sasa kama kisingizio kitakuwa hicho tena, wanachotakiwa sasa kuwa na huruma kwa wananchi.

Kwa upande wa wasafirishaji, najua kuwa ni muda mrefu wamekuwa wakihangaika kutaka kupandisha nauli na lilipokuwa suala hilo, ikawa ndiyo wamepata kisingizio, lakini kutokana na serikali kuingilia kati wanatakiwa kuangalia upya kwa kupunguza hata kama siyo kurudisha ile ya awali.

Sisemi kwamba warudishe ile ile ya awali, lakini angalau wapunguze nauli kidogo kwani na wao wamepunguziwa machungu ya bei ya mafuta ya serikali.

Haiwezekani serikali ipunguze bei, halafu wao wawe kimya kama vile hawajui kinachoendelea.

Wafanyabiashara wakifanya hivi watakuwa wamekwenda sawa na mawazo ya serikali ya kumjali mwananchi.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega (kulia), akizungumza na maofisa wa benki ya NMB, alipomtembelea banda la benki hiyo katika hafla ya kufunga Maonyesho ya Bodi ya Maziwa nchini yaliyofanyika kitaifa mkoani Katavi. Ulega, aliipongeza benki hiyo, kwa kukubali kutoa mikopo yenye riba ndogo ya asilimia tisa kwa mikopo wakulima na wafugaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watafiti Tanzania, Marekani wajadili mbinu kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Mary Geofrey**

WATAFITI na wanasayansi mbalimbali nchini kwa kushirikiana na Chuo cha Boston Massachusetts nchini Marekani, wamekutana kujadili mbinu za kutumia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mkutano huo ulifanyika juzi jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na watafiti walimu na wanafunzi 35 kutoka nchini Marekani, kujadili namna wanavyoweza kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kutumia watafiti na wanasayansi.

Watafiti waliohudhuria ni kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Chuo Kikuu cha Afya Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Chuo Kikuu cha Maji na watafiti kutoka Zanzibar.

Mkurugenzi wa Menejimenti na Maarifa wa COSTECH, Samson Mwera, alisema ugeni huo umekuja nchini kujifunza kuhusu mabadiliko ya tabianchi yanayotokea hasa kuangalia upande wa sayansi na utafiti. Alisema wanajifunza namna COSTECH wanavyotekeleza majukumu yake, kukutana na watafiti wenzao kwa sababu mabadiliko ya tabia nchi yameikumba maeneo mbalimbali duniani na kutembelea maeneo ya vivutio nchini.

"Wenzetu pia wamekuja kujifunza kuhusu sera zetu zinazohusiana na utafiti wa kisayansi na kuhakikisha kuwa mabadiliko ya nchi yanaweza kutekelezwa na kusaidia kwenye maendeleo ya kijamii na kiuchumi," alisema Mwera. Vile vile, alisema COSTECH wamekuwa wakifanya utafiti kwa kushirikiana na Wamarekani kubadilisha uwezo kutoka nchi hiyo na kujenga uhusiano.

"Kikubwa tumekuja kujenga uhusiano wa kisayansi kati ya Tanzania na Marekani kupitia chuo walichotoka," alisema.

Naye Mkufunzi kutoka MUHAS, Khadija Malima, alisema mabadiliko ya tabia ya nchi kwa wenzao wa Marekani wamekuwa wakifundishwa wanafunzi wa madarasa yote katika kuleta ufahamu.

Alisema wanategemea watajadili namna ya kushirikiana katika elimu namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Naye Mkurugenzi wa Utafiti na Mabadiliko ya Hali ya Hewa (TMA), Dk. Ladislaus Chang'a, alisema kwao ni fursa ya wataalamu kukutana na kujadili changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na fursa za kutumia katika kukabiliana nayo.

Alisema wataimarisha uhusiano wa kubadilishana utafiti na teknolojia ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani.

# DC amulika vikwazo kwa watoto wa kike

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Almas, amesema katika kuadhimisha Siku ya Hedhi Salama Duniani, jamii inatakiwa kutambua ina jukumu la kumaliza vikwazo vinavyowakabili watoto wa kike.

Fatma alitoa rai hiyo mkoani Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Namthamini Nasimama Naye' katika Shule za Sekondari Kibugumo na Kidete inayoendeshwa na vituo vya East Africa TV na East Africa Radio yenye lengo la kuchangisha taulo za kike kwa ajili ya kufikia wanafunzi 5,000 nchi nzima.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha watoto wa kike wanatatuliwa kero zinazowakabili, hivyo ni jukumu la jamii kuendelea kumuunga mkono. "Serikali chini ya Rais Samia imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha inamaliza changamoto zinazowakabili watoto wa kike nchini, ikiwamo kupata taulo za kike kwa ajili ya kujisitiri," alisema Fatma.

Aliwapongeza wadau wote wanaounga mkono jitihada hizo ikiwamo EATV na East Africa Radio kwa kuandaa kampeni hiyo inayolenga kumsaidia mtoto wa kike kujiamini na kuendelea na masomo bila vikwazo.

Mwakilishi wa EATV na East Africa Radio, Millicent Lasway, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, Regina Mengi, alisema kampeni ya Namthamini ilianza mwaka 2017 baada ya kupata taarifa kuwa wanafunzi wengi hushindwa kuhudhuria masomo kutokana na kukosa taulo za kike.

Alisema kampeni hiyo inawasaidia kuvunja ukimya kuhusu hedhi salama kwa kufika mikoa 15 ikiwamo Arusha, Kagera, Dar es Salaam, Lindi, Pwani, Tabira, Tanga na Singida.

Aliiomba serikali kuondoa kodi kwenye taulo za kike kwa kuwa uhitaji ni mkubwa, hasa kwa wanafunzi ambao wana ndoto za kufikia malengo yao. Alisema EATV na Radio wameshirikiana na wadau wengine katika kufanikisha kampeni hiyo, ikiwamo Klabu ya Rotary Osyterbay, CRDB, Amref Tanzania, RSK, HC Pads na Maji ya Kilimanjaro. Mwakilishi wa CRDB, Isaya Lyimo, alisema wamekuwa wakisaidia sekta ya elimu kwa kutoa vifaa vya kufundishia, kujenga madarasa na vifaa vya kujikimu katika siku za hedhi.

Alisema wameungana na wadau wengine kutoa msaada wa Sh. milioni tatu kwa ajili ya kuunga mkono kampeni hiyo.

Mwakilishi wa AMREF, Witness Katana, alisema wanatoa taulo za kike katika halmashauri 18 na wilaya 15 na kwamba kupitia kampeni hiyo, wamechangia Sh. milioni tano. Mwakilishi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Hellen Urio, alisema ni wadau wa hedhi salama na wanawajengea uwezo wanawake waliopo kwenye jamii kutambua kero mbalimbali zinazowakabili wanawake, ikiwamo hedhi salama. Alisema tayari katika halmashauri za Kisarawe, Mbeya DC, Kishapu na Ilala wameanza kutenga bajeti ya kununua taulo za kike na lengo ni kuhakikisha halmashauri zote zinaunga mkono suala hilo.

# Serikali kuanzisha vijiji kilimo kusaidia vijana

**Na Frank Monyo**

SERIKALI imesema ina mpango wa kuanzisha kijiji cha kilimo cha vijana na tayari imetenga ekari 20,000 katika wilaya za Chamwino na Bahi mkoani Dodoma kwa ajili ya mpango huo wa majaribio ambao unatarajiwa kuanza mwezi ujao.

Imesema itawaweka miundombinu yote ya kilimo na kwa kuanza vijana hao watalima alizeti kwa lengo la kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kula nchini.

Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, alibainisha hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kitabu cha mafanikio ya kilimo kwa vijana kitwacho Feed the Future.

Alisema siyo kweli kwamba vijana hawapendi kilimo, bali wanakabiliwa na vikwazo katika upatikanaji wa ardhi, pembejeo, uhakika wa masoko ya mazao yao na mtaji.

"Sisi kupitia programu yetu tunakwenda kutatua hizi kero, tunawatafutia ardhi ya kutosha, tunaweka miundombinu, tutawasaidia pembejeo, tutawasaidia kupata masoko ya mazao yao na mwisho wa siku tutaanzisha kijiji cha kilimo cha vijana ambapo vijana watafanya shughuli za kilimo na kuishi hapo kama eneo la makazi yao. Alisema hii ni dhamira njema ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa vijana na mpango huo unatarajiwa kufanyika nchi nzima.

Mavunde alisema ni muhimu kuwekeza katika maendeleo ya vijana ili kuharakisha mchakato wa uzalishaji kwa sababu wao ni idadi kubwa ya watu nchini.

Alisema kupitia mradi wa miaka mitano uliofadhiliwa na USAID (2017-2022) wa Feed The Future Tanzania Advancing Youths, umeunganisha vijana wenye umri wa miaka 15-35 katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Zanzibar.

Alisema vijana 33,000 wameongeza fursa za kipato kwa kuwaongezea uwezo wa kuajiriwa, ujuzi wa kibiashara, ujuzi wa uongozi na ushiriki.

"Watanzania wanashirikiana bega kwa bega na washirika wa kimataifa na tunakaribisha uwekezaji zaidi katika Sekta ya Kilimo. Tunaamini kuwa kukuza sekta ya kilimo ndiyo ufunguo wa kufungua uchumi wa Tanzania," alisema Mavunde na kuongeza:

"Nimefurahi kusikia kwamba katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi wa kuwaendeleza vijana, mmepata fursa za kuendesha uchumi wa vijijini, na tunaona haya kwa mafanikio yaliyopatikana kwa vijana. Ninyi ni injini ya ukuaji na tunaona ustawi, tunajua kwamba taifa letu liko mikono salama ya vijana wakulima." Alisema Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetoa zaidi ya ekari 200 za ardhi na Sh. milioni 400 kwa ajili ya Mradi wa Maendeleo ya Vijana (AY) na itaendelea kuwekeza na kusaidia vijana hata baada ya AY kumalizika.

Mkurugenzi wa Misheni wa USAID/Tanzania, Kate Somvongisiri, alisema uzinduzi wa kitabu hicho ni kielelezo cha mafanikio ya shughuli ya kilimo ambayo imefanywa kwa ustadi mkubwa na vijana wa Kitanzania.

"Marekani inajivunia na kuheshimiwa kusherehekea zaidi ya miaka 60 ya ushirikiano na Serikali ya Tanzania. Serikali ya Marekani kupitia USAID inatoa vipaumbele vya uwekezaji kwa vijana," alisema. Mkuu wa Vijana wa Taasisi ya Advance Youth Party (COP), Ngasuma Kanyeka, alisema hadithi za mafanikio ya kilimo kwa vijana ilikuwa msingi wa uwekezaji wa USAID uliolenga kuwafikia vijana na kuboresha maisha.

Alisema mradi wa AY imefikia vijana 42,000 ndani ya miaka mitano ilhali lengo lilikuwa kuwafikia vijana 33,000.

# 'Usafi mazingira uanzie familia'

**Na Jenifer Gilla**

KATIBU Tarafa wa Mbagala, Bertha Minga, amesema suala la usafi wa mazingira linatakiwa kuwa agenda kuanzia ngazi ya familia ili kufanikisha lengo la kuyatunza katika nkoa wa Dar es Salaam.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uzinduzi wa Wiki ya Mazingira Duniani kimkoa, uliofanyika katika stendi ya mabasi yaendayo Kusini, Temeke mwisho kwa ushirikiano na Manispaa ya Temeke na wadau wa mazingira. Akimwakilisha Mkuu wa wilaya hiyo, Jokate Mwegelo, Katibu tarafa huyo alisema serikali ina wajibu wa kuhakikisha jamii inaishi katika mazingira salama, ndiyo maana inaweka magari kila mitaa kwa ajili ya kukusanya taka na kuwasihi wananchi kulipa ada bila kushurutishwa ili usafi katika wilaya hiyo uimarike.

"Namna pekee ya kuhakikisha usafi katika wilaya yetu unaimarika ni kushiriki katika kutoa ada za taka, hii ni sheria yetu ndogo ili taka zetu zichukuliwe na kupelekwa dampo," alisema.

Alisema Idara ya Mazingira katika wilaya hiyo itatoa ushirikiano wa kutosha kwa wadau wa mazingira ili usafi unakuwa ni tabia endelevu.

"Nataka niwaambie kwamba tupo bega kwa bega na ninyi, kuhakikisha suala hili linakwenda kufanyika na hatimaye Temeke tunayoitaka, safi na inayopendeza tunakwenda kuiona kwa pamoja," alisema.

Alisema ili kutekeleza jambo hilo kila mmoja anapaswa kuwa balozi wa usafi kwa kuhakikisha anaelimisha pale mtu anapotupa taka ovyo ili Temeke na Dar es Salaam kwa ujumla iwe safi. Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi wa Mazingira katika Manispaa Temeke, Husna Mrisho, alisema wakiwa wenyeji wa maadhimisho hayo kimkoa wameona umuhimu wa kuzindua kwa kutoa elimu ili wananchi wa eneo hilo wajifunze umuhimu wa kutunza mazingira. "Tumechagua eneo la stendi ya mabasi yanayoenda kusini na kufanya usafi ili kuongeza hamasa na ari ya kufanya usafi kwa wananchi wote, kwa kuwa hii ni stendi kubwa kwa manispaa hii," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Azimio, Amina Ismail, alisema ameungana na wadau pamoja na viongozi wa manispaa hiyo ili kutoa hamasa kwa vijana wa wilaya kutunza mazingira na kuiunga mkono serikali katika suala hilo. "Sisi kama madiwani kuwahimiza wananchi wetu kufanya usafi ni jambo muhimu na nina amini mafunzo ya leo wameyafurahia na litakuwa suala endelevu kwao," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Wadau wa Mazingira Wilaya ya Temeke, Innocent Mahendeka, alisema lengo la shughuli hiyo ni kutoa elimu kwa wananchi wa eneo hilo kuhusu Siku ya Mazingira Duniani na umuhimu wa kuweka mazingira safi.

Alisema wamechagua kufanyia katika stendi hiyo ili kufikisha ujumbe kwa abiria wanaosafiri kwenda mikoa ya Kusini wakifika huko watunze mazingira ya barabara wanazopita.

"Wasafiri wamezoea kupewa elimu ya usalama barabarani, lakini mazingira yanasahaulika, leo tukasema hapana tujenge makundi yote, ili hata hawa wanaosafiri wapate elimu, lakini wananchi pia waijue Siku ya Mazingira na kuitekeleza," alisema.

Mwakilishi kutoka Taasisi ya Mabalozi wa Usalama Barabarani, Irene Mselemu, alisema wameguswa kushiriki ufunguzi huo kuhamasisha abiria kuacha kutupa taka barabarani wanapokuwa safarini.

"Tupo hapa kama wadau wa usalama barabarani kuwaelimisha wananchi namna ya kuvitumia vizuri vile vyombo ambavyo vimewekwa katika magari kwa agizo la kisheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA). Hivyo abiria wanaotumia mabasi hayo wana wajibu wa kutunza mazingira kwa kuweka taka kwenye vyombo hivyo. Alisema mazingira yanapotunzwa husaidia jamii kuwa na afya njema kwa kuwa wanapata hewa nzuri, pamoja na kuepukana na magonjwa ya milipuko kama kipindupindu. Balozi wa mazingira kutoka Ofisi ya Makamu waRais, Muungano na Mazingira akiiwakilisha wilaya hiyo, Richard Kalongole, alisema ni jambo la kutia moyo kuona Temeke inaamka katika suala la usafi wa mazingira hali inayo onyesha wilaya hiyo imedhamiria kuweka mazingira yake safi.

Maadhimisho ya siku hiyo kimkoa yatafanyika Juni 5, 2022 katika viwanja vya Mbagala Zakhiem na wilaya hiyo itakuwa mwenyeji.

# Wazalishaji maziwa watakiwa kuthibitisha ubora wa bidhaa

**Na Mwandishi Wetu,**
MPANDA

WAZALISHAJI wa maziwa na bidhaa zake wameshauriwa kuthibitisha ubora hatua ambayo itawasaidia kuwaongezea masoko na tija.

Ushauri huo ulitolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Azimio, mjini hapa kuanzia Mei 27 na kumalizika juzi.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, Ofisa Uhusiano wa TBS, Neema Mtemvu, alisema washiriki hao na wazalishaji wanatakiwa kuthibitisha ubora wa maziwa na bidhaa zake ili kupata manufaa kiuchumi na masoko ndani na nje ya nchi.

Alisema TBS imeshiriki maonyesho haya kwa lengo la kuwasogezea huduma karibu wazalishaji wa maziwa kwa kuwapatia elimu ya viwango ili kuzalisha bidhaa bora na salama zinazoweza kushindana katika soko la kitaifa na kimataifa.

Hiyo ni kwa sababu nchi za Afrika Mashariki zina makubaliano kuhusiana na bidhaa zilizothibitishwa ubora ambapo kila mzalishaji aliyethibitisha ubora wa bidhaa yake ni ruksa kupeleka bidhaa hizo katika nchi yoyote katika ukanda huo bila kukumbana na vikwazo vya kibiashara.

"Huduma ya uthibitishaji ubora wa bidhaa kwa wajasiriamali wadogo ni bure kabisa, kinachotakiwa ni wajasiriamali kupata barua ya utambulisho kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na kuipeleka TBS, ambapo mchakato wa kuwapatia alama ya ubora unaanza mara moja," alisisitiza Mtemvu.

Alisema TBS inatambua mchango wa wajasiriamali katika kukuza pato la taifa na kutengeneza ajira kwa wananchi wengi, ndiyo maana kuna mchakato endelevu wa kutoa elimu kwa wajasiriamali kwa kuwa na hilo ni sehemu ya majukumu ya shirika ili waweze kupata alama ya ubora.

Pia alisema kupitia maonyesho hayo walitoa elimu kwa wananchi kuhusiana na masuala ya viwango na kuwataka waelewe kwamba vita ya bidhaa hafifu sio ya TBS pekee, bali ni jukumu la kila mwananchi.

Alisema wananchi hao walielimishwa umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku pamoja na kuwafahamisha fursa ya huduma ya kuthibitisha bure bidhaa za inayotolewa kwa wajasiriamali wadogo.

Kwa mujibu wa Mtemvu, mbali na kutoa elimu kwa wananchi hao kuhusu masuala ya viwango wametakiwa kuhakikisha wanakuwa mabalozi kwa kuhamasisha kutumia bidhaa bora katika jamii wanayoishi.



Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo (kulia), akizungumza na wateja wa benki hiyo, mkoa wa Shinyanga juzi, wakati wa hafla ya chakula maalum kwa ajili yao, iliyolenga kujadili fursa za kibiashara, mipango ya ukuaji na huduma zitolewazo na Exim mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TARI yakunwa shule kitalu cha matunda

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeridhishwa na maendeleo ya kitalu cha miche ya matunda katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Arusha, jijini hapo.

Meneja wa TARI Kituo cha Tengeru, Dk. Shimwela Mpoki, alieleza kuridhishwa huko jana baada ya kufanya ziara katika shule hiyo.

Akizungumza shuleni hapo, Dk. Mpoki alisema ziara hiyo ni matokeo ya makubaliano kati ya TARI na Ofisi ya Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, ya kusaidia kusambaza takribani miche 30,000 katika shule mbalimbali za Jiji la Arusha kwa lengo la kustawisha na kuboresha mazingira na lishe kwa wanafunzi.

Katika ziara hiyo, wataalamu kutoka TARI Tengeru walipata fursa ya kutoa ushauri wa kitaalamu kwa uongozi wa shule hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya uchimbaji mashimo na uwekaji mbolea ili miche hiyo ipandwe na kuleta matokeo chanya.

Shule ya Sekondari ya Wasichana Arusha ilipata miche 1,415 ya matunda mbalimbali, huku kazi ya kugawa miche katika shule zingine mkoani Arusha zikiwa zinaendelea.

Kutokana na hatua hiyo, uongozi wa shule hiyo ulishukuru TARI kwa juhudi inazofanya kusaidia jamii na kuahidi ushirikiano zaidi katika utunzaji wa miche hiyo ili ilete matokeo tarajiwa. Uongozi huo ulisema kampeni za upandaji miti katika shule utaboresha lishe za wanafunzi shuleni hapo na kustawisha mazingira ya shule na Jiji la Arusha kwa ujumla.

Katika hatua nyingine, Dk. Mpoki alitumia ziara hiyo kuupatia uongozi wa shule hiyo mbegu za mboga mbalimbali zikiwamo mchicha pori, akeri, nguruma na nyanya chungu aina ya Tengeru White na DB3. Lengo la kugawa mboga hizo ni kuwasaidia wanafunzi kupata virutubisho vinavyotokana na mboga ili kuboresha lishe ya wanafunzi shuleni hapo.

Alisema hatua hiyo ya ugawaji miche na mbegu katika shule hiyo ni sehemu ya mpango wa TARI kuhakikisha teknolojia zilizofanyiwa utafiti zinawafikia walengwa ili kuongeza tija na uzalishaji katika kilimo.

Dk. Mpoki aliongeza kuwa TARI Tengeru inajipanga kutoa elimu katika shule hiyo ya jinsi ya kupanda miche na mbegu hizo kwa kufuata kanuni za kilimo bora.

TARI inachangia ufikiwaji wa malengo ya programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo (ASDP) na ufikiwaji wa maazimio ya Malabo katika kuondoa umaskini na njaa kupitia kilimo na kutunza mazingira.

HABARI KITAIFA

## ‘Serikali izuie bidhaa za plastiki kuingizwa’

**Na Gwamaka Alipipi**

OFISA Programu Mkuu wa Taasisi ya Agenda inayojihusisha na utunzaji wa mazingira, ameishauri serikali kukomesha uingizwaji wa taka za kielektroniki nchini na vifaa vya plastiki kama vile vya jikoni, ofisini, midoli, vibanio vya nywele kwa kuwa zina athari kubwa kwa afya ya binadamu.

Silvani Mng'anya ametaja athari za bidhaa hizo zinajumuisha magonjwa ya saratani, athari katika ubongo, kinga za mwili kushuka pamoja na mfumo wa homoni za uzazi kuharibika.

Alitoa ushauri huo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu athari za matumizi ya bidhaa za plastiki.

Mng'anya alisema Bara la Afrika limegeuzwa kuwa sehemu ya kupeleka taka zenye sumu kinyume cha sheria na bidhaa hizo zimekuwa na athari kubwa kwa binadamu ikiwamo kuharibu ubongo, magonjwa ya saratani, kuharibu mfumo wa homoni pamoja na kushusha kinga ya mwili.

"Utafiti uliofanywa na maabara huru katika nchi ya Jamhuri ya Czech, umebaini kuwa bidhaa nyingi za plastiki kama vile midoli, vifaa vya jikoni, vifaa vya ofisini, vitana na vibanio vya nywele na vinginevyo vilivyotengenezwa kwa kutumia plastiki zilizorejelezwa zina viwango vikubwa vya kemikali," alisema Mng'anya. Vilevile, ofisa huyo alisema ripoti ya utafiti uliofanywa katika nchi 11 za Afrika na Uarabuni na kutolewa na asasi ya Arnika pamoja na mtandao wa kimataifa wa IPEN, umebaini bidhaa 61 zilizozalishwa kwa plastiki zina viwango vikubwa vya kemikali inayopunguza uwezekano wa bidhaa kuwaka moto.

Mng'anya alizitaja nchi hizo kuwa ni Tanzania, Burkina Faso, Misri, Ethiopia, Gabon, Cameroon, Tunisia, Morocco, Kenya, Syria na Jordan, akisema sampuli hizo zilifanyiwa uchunguzi kwa kutumia mionzi ya x-ray ili kubaini kemikali sumu kwenye bidhaa za plastiki.

Mng'anya alisema: "Taka za kielektroniki na vifaa vya plastiki kutoka kwenye magari yaliyokwisha muda wake vyenye viwango vikubwa vya kemikali sumu za kuzuia kuwaka kwa moto, zinapaswa kuzuiwa kuingia katika mnyororo wa urejelezaji.

"Kuongezeka kwa kemikali hizi hatarishi kama dutu kutaendelea kuhatarisha afya ya mwanadamu kwa miongo mingi."

# TAKUKURU yaokoa vifaa tiba

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro imefanikiwa kuokoa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 26 kufuatia baadhi ya waganga wafawidhi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na mkoa kufanya ubadhirifu huo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro, Manyama Tungaraza, alisema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya kukamatwa na kuokolewa kwa dawa na vifaa tiba hivyo na kuzikabidhi kwa uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

Tungaraza alisema dawa na vifaa tiba hivyo zilinunuliwa na hazikupelekwa katika maeneo husika kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa.

Alisema ukaguzi maalum uliofanywa na timu iliyoundwa na timu ya usimamizi na uendeshaji wa huduma za afya Mkoa wa Morogoro, ulibaini katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 malipo ya Sh. milioni 51 yalifanywa kwa Mshitiri wa Bahari Pharmacy kwa ajili ya kulipia dawa, yahakuwa halali kwa kuwa hayakufuata taratibu za ununuzi. Tungaraza alisema kuwa baada ya kufanya uchunguzi wa kina, ilibainika kuwa Aprili 16, 2021 malipo yenye thamani ya Sh. milioni 51 yalifanywa kwa kampuni (mshitiri) ya Bahari Pharmacy kwa ajili ya malipo ya dawa na vifaa tiba.

Alisema kuwa wakati malipo hayo yanafanyika, hakukuwa na nyaraka halali kwa ajili ya malipo, bali yalifanyika kwa kutumia hati ya awali ya malipo ya mshitiri ambayo ilikuwa na thamani ya Sh. 54,018,509 pamoja na hati ya mauzo kutoka Bohari ya Dawa (MSD) yenye thamani ya Sh. milioni 70.

Tungaraza alisema kuwa baada ya malipo hayo kufanyika Aprili 20, 2021, Bahari Pharmacy aliandika 'Delivery Note' pamoja na 'Tax Invoice' kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro nyaraka hizo zikiwa na jumla ya aina 38 tu ya dawa na vifaa tiba tofauti na aina 63 zilizoko katika hati ya awali ya malipo (profoma invoice).

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa alisema ukaguzi wa dawa na vifaa tiba ulifanyika Aprili 21, mwaka jana (2021) zikiwa zimepita siku saba tangu kufanyika kwa malipo ya Sh. milioni 51 ambao ulibaini kuwa dawa hizo zilikuwa na thamani ya Sh. 25,428,212.

Tungaraza alisema wakati Kamati ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro inafanya ukaguzi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi pamoja na vifaa vingine, Aprili 21, mwaka jana (2021) kutoka Bahari Pharmacy vyenye thamani ya Sh. 25,428,272, tayari malipo ya Sh. milioni 51 yalikuwa yamefanyika kwa mshitiri huyo Aprili 26, mwaka jana.

"Katika uchunguzi tuliofanya, tulibaini kwamba dawa na vifaa tiba yenye thamani ya Sh. milioni 26 hazikupokelewa, TAKUKURU ilimtaka mshitiri aitwaye Bahari Pharmacy arejeshe dawa na vifaa tiba, hivyo ambapo leo (Mei 30, 2022), tunakabidhi kwa uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro ili zitumike katika kutibu na kuokoa maisha ya wananchi," alisema Tungaraza.

Mkuu huyo alitoa wito kwa watumishi wote wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na ya rufani kuzingatia Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2013 na kuzingatia taratibu za utumishi wa umma kwa kuwa waadilifu na waaminifu wakati wanatekeleza majukumu yao.

Tungaraza alisema taasisi hiyo haitasita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wale wote watakaobainika kwenda kinyume cha taratibu zilizowekwa za ununuzi wa umma na utumishi wa umma.




Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), akisalimiana na baadhi ya wateja wa benki hiyo wakati wa chakula cha usiku kilichoandaliwa na benki hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mkakati kukabili vifo vya watoto waanikwa

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau wa afya, imezindua BiliDx - kifaa cha kibunifu na cha bei nafuu ambacho hutambua mara moja viwango vya bilirubini katika seramu kutoka tone dogo la damu linalowekwa kwenye ukanda wa mtiririko unaoweza kutumika kwa urahisi.

Inafafanuliwa kitaalamu kuwa hyperbilirubinemia ya watoto wachanga huathiri mamilioni ya watoto wachanga kila mwaka barani Afrika na ni sababu kuu ya vifo vya watoto wachanga na ulemavu kwa kundi hilo kwenye nchi za kipato cha chini na cha kati.

Mkurugenzi Msaidizi Afya ya Uzazi na Watoto Wizara ya Afya, Dk. Ahmad Makuwani, alibainisha hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa kifaa hicho jijini Dar es Salaam.

Alisema Shirika la Hatch Technologies likishirikiana na mpango wa NEST360 unaotekelezwa na Anudha Limited-Tanzania, Taasisi ya Afya Ifakara na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na Wizara ya Afya, lina lengo la kupunguza vifo vya watoto wachanga kwa kuhakikisha vifaa tiba vyenye ubora na vinavyoweza kutumika katika mazingira yenye rasilimali ndogo, vinapatikana kwa bei nafuu.

Alisema Hatch pia inashirikiana na Anudha kusambaza vifaa tiba vya watoto wachanga na kupitia mradi wa NEST360 na tayari vifaa tiba hivyo vimeshasambazwa katika hospitali saba za awamu ya kwanza ya mradi kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) tawi la Upanga na Mloganzila.

Vilevile, zimo hospitali za rufani za Amana, Mwananyamala na Temeke. Hospitali zingine ni za Kanda KCMC, Moshi na Mbeya.

"Hiki ni kifaa cha gharama nafuu cha huduma ya uchunguzi ambacho hutathimini mara moja jumla ya viwango vya bilirubini katika sehemu kunakotoka tone dogo la damu nzima, hii inafanya BiliDx kuwa na gharama nafuu na njia ya haraka na nafasi kugundua hyperbilirubinemia ya watoto wachanga katika mipangilio ya rasilimali ya nchi kwa sababu hahitaji 'centrifuge' tofauti na bilirubinomita za kawaida," alisema.

Alifafanua kuwa moja ya sababu kuu zinazochangia vifo vingi vya watoto wachanga kutokana na hyperbilubinemia nchini, ni kiwango kikubwa cha watoto wanaozaliwa nje ya hospitali.

"Kwa kuzingatia kwamba tathmini ya kuona hyperbilubinemia mara nyingi haitoshi kufahamisha utambuzi sahihi, BiliDx hutoa zana inayotegemewa, inayoshikiliwa kwa mkono kwa matukio haya kwa sababu inabebeka sana, yenye ufanisi na haina gharama kubwa," alisema. Pia alitoa rai kwa wadau wote wa afya ya mama na mtoto kuendelea na juhudi za uimarishaji wa afya ya mama na mtoto ikiwamo kutumia vifaa tiba vyenye ubora na ufanisi mkubwa kwa ajili ya matibabu ya watoto wachanga wanaozaliwa na uzito pungufu.

"Juhudi hizo ziende sambamba na ukusanyaji na matumizi ya takwimu katika kuboresha huduma katika vituo vya kutolea huduma ngazi zote.

"Ni wajibu wa wananchi, wazazi na walezi kuhakikisha mjamzito anajifungulia katika kituo cha kutolea huduma za afya na mtoto mchanga mgonjwa anapata huduma stahiki kwenye vituo vya kutolea huduma," alihimiza.

Ripoti zinaonyesha watoto wachanga wanaozaliwa kwenye nchi za Kusini mwa Jangwa la Saharan Africa na Kusini mwa Asia wako hatarini mara 10 zaidi kupoteza maisha ndani ya mwezi mmoja tangu kuzaliwa ikilinganishwa na nchi zenye kipato kikubwa kutokana na kutokupata huduma za matibabu. Asilimia 75 ya watoto njiti wanaweza kuokolewa kwa kupatiwa matibabu stahiki.

Catherine Paul, Mkurugenzi Mkazi wa NEST360 alisema programu hiyo inalenga kupunguza vifo vya watoto wachanga kusini mwa Jangwa la Saharan kupitia utoaji wa teknolojia ya kulinda afya ya watoto wachanga, kutoa elimu kwa wanaohudhuria kliniki na watoa huduma za afya namna ya kutumia vifa hivyo vya kiteknolojia.

Mkrugenzi huyo pia alisema wanatoa msaada kwa wabunifu wazawa kuja na teknolojia ambayo itafanya vizuri kulingana na maeneo waliyomo.

# Serikali sasa kujenga miundombinu vyuo vikuu

SERIKALI kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Uchumi (HEET), imebainisha namna itakavyojenga miundombinu kwenye vyuo vikuu nchini ili kukabiliana na ongezeko kubwa la wanafunzi.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Paulina Nahato, aliyehoji serikali ina mpango gani wa kuongeza miundombinu ya vyuo vikuu nchini kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi.

Akijibu swali hilo, Kipanga alisema kupitia mradi huo kutajengwa chuo kikuu kipya cha kilimo na teknolojia cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Butiama chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 5,620.

Pia alisema mradi utajenga kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Mkoa wa Lindi chenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 360, kampasi mpya ya Mloganzila ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (11,000), kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ya Mizengo Pinda Mkoa wa Katavi (2500), kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Mkoa wa Rukwa (3000).

Vilevile, alisema mradi wa HEET utafanya ujenzi wa kampasi mpya za vyuo vikuu katika mikoa ya pembezoni (marginal satellite cities) ikiwamo Kagera, Tanga, Kigoma, Shinyanga, Mwanza, Simiyu, Ruvuma, Manyara na Singida.

Alisema mradi huo kwa ujumla unatarajia kuziboresha Taasisi za Elimu ya Juu 19 kwa kujenga hosteli 34 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 9,042, vyumba vya mihadhara 130 (27,254), maabara/karakana (7,850), kumbi za mikutano ya kisayansi 23, miundombinu ya mashambani pamoja na vituo atamizi 10.

Katika swali lake la nyongeza mbunge huyo alisema pamoja na jitihada za serikali kuongeza miundombinu inayoendelea, bado kuna fani hazitolewi nchini na kuhoji serikali haioni haja ya kushirikiana na vyuo vya nje ili kutoa kozi hizo hasa ya afya.

“Pamoja na mkakati wa miundombinu serikali ina mpango gani wa kuongeza wahadhiri nchini,” alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Kipanga, alikiri baadhi ya kozi kwenye sekta ya afya hazitolewi nchini na kwa muda mfupi serikali imepata uzoefu kupitia janga la UVIKO-19, wanafunzi wengi walirejeshwa nchini na pia vita ya Ukraine na Urusi.

Alisema wanafunzi hao wanasoma kozi ambazo hazipo nchini na serikali imeanza mjadala wa kuangalia namna ya kushirikiana na vyuo vya nje ili kozi hizo zitolewe kwa ushirikiano.

“Kupitia mradi wa HEET tunakwenda kusomesha wahadhiri wapya zaidi ya 1,000 pamoja na uongezaji wa miundombinu utakwenda sambamba na kuwasomesha wahadhiri na kwa awamu ya kwanza watakuwa wahadhiri 625 kwa kozi ndefu na kwa kozi fupi wahadhiri zaidi ya 400, ili kupunguza uhitaji huo kwenye vyuo,” alisema.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi (kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), George Simbachawene, baada ya kuahirishwa kwa Bunge dakika 30 kutokana na kutokuwapo kwa Waziri wa Nishati, Januari Makamba na Naibu wake, Stephen Byabato, wakati wa kuchangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kanuni kudhibiti bei za dawa zawekwa mezani

BUNGE limeelezwa kuwa kwasasa serikali imeandaa kanuni za kudhibiti bei za dawa na tayari zimewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Naibu Waziri wa Afya, Dk.Godwin Mollel alieleza hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwanaisha Ulenge.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kutoa bei elekezi ya vifaa vya tiba hasa vya macho, pua na koo.

Akijibu swali hilo, Dk.Mollel alisema bei elekezi za vifa tiba zitaandaliwa baada ya kukamilika kwa kanuni za bei za dawa elekezi.

Katika swali la nyongeza mbunge huyo alisema anapozungumzia vifaa tiba vya macho, pua na koo anamaanisha ongezeko la watu wasiosikia (viziwi) na wasioongea (mabubu).

“Je, serikali haioni haja ya kupeleka vifaa vya kupima usikivu kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ili kila mtoto anayezaliwa apimwe usikivu na kupunguza tatizo la viziwi na mabubu nchini,” alihoji.

Alihoji mwaka 2016/17 serikali ilianzisha upandikizaji wa vifaa vya usikivu nchini na kuhoji serikali ina mpango gani wa kuongeza vitengo vya kushughulikia tatizo hilo.

Dk. Mollel akijibu maswali hayo, alisema serikali imepokea ushauri huo wa mbunge na kwamba katika kifurushi cha mama anayejifungua kitazingatia hilo ili afanyiwe uchunguzi kuwatambua mapema na kuwasaidia.

Alisema serikali itasogeza huduma hiyo ya uwekaji wa vifaa vya usikivu itasogezwa hadi hospitali za mikoa.




Habari zote na Augusta Njoji

# Vikundi vya vijana vyakopeshwa bilioni 13.5/-

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema kwa mwaka wa fedha 2021/22 vikundi 1,441 vya vijana vilikopeshwa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 13.5 nchini.

Naibu Waziri wa ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda.

Mbunge huyo alihoji serikali ina kauli gani kuhusu mikopo inayotolewa na halmashauri kwa kuwa mfumo unawaacha nje vijana wengi kwa kukosa sifa za kupata mikopo hiyo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Dk. Dugange alisema kanuni ya sita ya kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ya mwaka 2018 pamoja na marekebisho yake inaelekeza sifa na vigezo vya kuzingatiwa kwenye utoaji mikopo kwa vijana.

“Vigezo na sifa hizo ni pamoja na kikundi kinachofanya shughuli za ujasiriamali au kinachotarajia kuanza shughuli hizo, kikundi kiwe kimetambuliwa kama kikundi cha vijana, wanakikundi wawe Watanzania wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35, kikundi cha vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano na kuendelea, kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya kikundi na kikundi hakitajumuisha wajumbe wenye ajira rasmi,” alisema.

Kuhusu kauli ya serikali, alisema vijana wenye sifa tajwa waendelee kujiunga katika vikundi vya wajasiriamali na kuomba mikopo hiyo ili kuinua uchumi wao.


Katika swali lake la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zainab Katimba, alihoji serikali ina mkakati gani wa kufanya ulezi kwa vikundi hivyo vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili viwe na ufanisi katika shughuli zake.

“Tathmini inaonyesha malipo ya fedha hizi za mikopo zinazotolewa na halmashauri bado zinasuasua, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mikopo hii inalipwa kwa wakati ili inufaishe wengi zaidi,” alihoji.

Akijibu maswali hayo, Dk. Dugange alisema mkakati ambao serikali imekuwa ikiufanyia kazi ni katika kuhakikisha vikundi hivyo vinakuwa endelevu na tija ni maofisa maendeleo ya jamii kuwatembelea mara kwa mara kufanya mafunzo ili vikope na kurejesha kwa tija.

Alikiri kuwapo kwa tatizo la kuchelewa kutolewa fedha na inatokana na vikundi kutokidhi vigezo vinavyotakiwa.

Ukurasa 13




Watanzania tulipie elimu au matibabu?

# BUFE

IJUMAA JUNI 3, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




## Rais Samia alivyoonyesha kasi uwekezaji kupenya sakafu ngumu kwa muda mfupi

Ukurasa 12

# Wanakijiji ghafla wageuka wawekezaji baada ya mashamba yao kupata hati

**Na Renatha Msungu, Bahi**


Wanavijiji wa mkoani Dodoma, siku walipokabidhiwa hati zao za makazi. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

HIVI Karibuni serikali kupitia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), ilitoa hati 2890 za mashamba kwa wakazi wa vijiji vya Msisi na Makanda vilivyopo wilayani Bahi mkoani Dodoma.

Hati hizo ni za mashamba ambayo awali walimiliki bila ya hati, kutokana na kutofikiwa na mpango huo. Sababu kuu zinajumuisha, wengi kutokujua undani wa umuhimu mtu kuwa na hati ya eneo analomiliki.

Lakini hivi sasa, baada ya kukabidhiwa hati hizo, wanaonekana kufunguka macho kwa kutazama fursa zilizopo, kwa ajili ya kujiinua kiuchumi kupitia mikopo ambayo watakopeshwa na taasisi za fedha.

### WANUFAIKA WA MRADI

Maria Mpole, ni mnufaika wa hati kutoka serikalini baada ya kurasimishwa mashamba yao, akisema zitawainua kiuchumi,kutokana na kwamba watazitumia kuchukua mikopo ya kuendeleza kilimo chenye tija, akifafanua baada ya kukabidhiwa hati, tayari wana vitega uchumi vya kuwasaidia kukopa katika taasisi za fedha kama benki, hata wakaboreshe kilimo vijijini.

Anasema kwa sasa wanajikita kufanya kilimo chenye tija, ili kuhakikisha wanasonga kiuchumi, kutokana na kwamba wana nyenzo zinazowasaidia kupata mikopo.

"Nashukuru serikali hivi sasa inawaona wakazi wa vijijini kwa kuwapa hati. Hati,hii inatusaidia kupiga hatua kwenye kilimo tunachofanya," anasema Mpole.

Anasimulia, awali kabla ya kuwa na hati ilikuwa ngumu kwao kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha, lakini sasa vikwazo hivyo wameondoshwa, wakitetewa na hati zao halali wanazomiliki

.Pia, Elizabeth Abdallah, anasema awali iliwawia vigumu kupata mikopo kutoka benki walikuwa na mashamba, lakini sasa wanatembea kifua mbele kwa kuwa wana uwezo kukopesheka kwenye taasisi za fedha, siri kuu ni mashamba hayo kukosa hati miliki.

### MKURUGENZI MKURABITA

Mkurugenzi Mtendaji wa MKURABITA, Dk. Seraphia Mgembe, anasema jitihada za serikali kurasimisha mashamba na kuwapa hati wananchi wa vijiji hivyo, ni moja ya vyanzo vya kupiga hatua kiuchumi katika mambo mbalimbali wanayofanya.

Hapo anafafanua kwamba katika uhalisia huo, mtu akimiliki hati ya mashamba aliyokuwa nayo,tayari

anahesabika ni mwekezaji kwa sababu anakuwa na uwezo wa kuingia taasisi za fedha kukopa.

Dk. Mgembe anataja udhamini wa hati yake ya ardhi, umemsaidia kupata mtaji wa biashara na kilimo chenye tija, akishuhudia matokeo chanya, kwake na taifa lake, hivyo wakazi wa vijiji waliopata hati wako katika nafasi nzuri kuinuka kiuchumi.

Pia, anaeleza kilichofanyika ni hatua endelevu, kwani itaendeshwa katika maeneo mengine, akiwataka wananchi wa vijiji vitakavyonufaika na fursa tajwa kujiunga haraka na hatua za maendeleo yao maana watakuwa wamewezeshwa na ni wajibu wao kuunga mkono jitihada za serikali katika maendeleo yao.

### WAZIRI MHAGAMA

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, anasema mtu anapokuwa na ardhi yenye hati, maana yake iko salama, pia inakuwa sehemu ya vitega uchumi.

"Naomba msibaki nyuma kutumia fursa ya urasimishwaji wa mashamba unaofanywa na serikali, changamkieni fursa ya kupata hati za mashamba mliyokuwa nayo, ili kuondokana na bugudha ya hapa na pale ya kugombea ardhi," anasema Waziri Jenista.

Hata hivyo, waziri ana angalizo kwamba wanaokopeshwa wajipange kutumia fedha kwa ajili ya maendeleo na sio kufanyia sherehe za kimila, zitakazowarudisha nyuma kimaendeleo.

Waziri pia anakumbusha kuwa, wakati serikali inaleta mageuzi katika sekta ya kilimo, wakulima nao watumie fursa zinazoibuliwa kubadilika kifkra katika maendeleo yao, akiwapa mfano wana - Bahi hao kujitosa katika kilimo cha mazao kama mtama na alizeti, ambavyo vimekamata soko.

### SERIKALI BAHI

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mukunda, anaipongeza serikali kuwapatia wananchi wa eneo hilo, pia hati za mashamba zitakazowasaidia kufanya maendeleo hata wakainuka kiuchumi.

Mkunda anasema, kwake kiongozi mkuu wa wilaya hiyo, anaahidi watahakikisha wananchi wake wanapata

uelewa stahiki na muhimu na akawahimza pia wafanye maendeleo, pasipo kubweteka .

Diwani wa Kata ya Msisi, Mathayo Malilo, anaiomba serikali kuendelea kutoa elimu kwa wakazi wa vijiji vya mbali, umuhimu wa kuwa na hatimiliki za mashamba, kwani wengi wamekuwa hawazingatii na sababu kuu ni uelewa duni.

"Tunaomba serikali izidi kutoa elimu kwa wananchi wa vijiji mbalimbali juu ya umuhimu wa kuwa na hati za mashamba ili ziwasaidie kuwajengea uwezo," anasema Diwani Malilo.

Mbunge wa Bahi, Keneth Noro, anaiomba serikali kuendelea kurasimisha mashamba katika vijiji ambavyo bado havijafikiwa na mpango huo, kupanua wigo wa wanufaika wenye ardhi salama.

UCHUMI

# Rais Samia alivyoonyesha kasi uwekezaji kupenya sakafu ngumu kwa muda mfupi

- Kimataifa kagonga hodi, kafunguliwa kwa mabilioni
- Aleta ufunguo unaofungua ajira, mzunguko wa pesa

**Na Peter Orwa**

NI mwaka mmoja na 'ushee' sasa tangu Rais Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani. Hadi kuadhimisha mwaka mmoja wa utendaji wake, kuna mengi alishayaanza tangu alipopewa jukumu.

Imedumu kuwa staili kitaifa, uongozi kupokezana kijiti katika kuendeleza mfumo wa kujenga uchumi na maendeleo kitaifa wakitumikia ajenda ya pamoja. Nchini Tanzania inashuhudiwa kwa awamu sita za uongozi.

Hata hivyo, kama ilivyo hulka ya binadamu yeyote na kote duniani, suala la kujenga uchumi lina maana pana na kila kiongozi huja na upekee wake katika utashi wa namna ya kufanikisha ajenda ya pamoja ya kijiti walichopokezana.

Hivi sasa Tanzania iko chini ya uongozi wa mwanamke, Rais Samia na hata kupata jina la 'Mama.' Kati ya mambo aliyoanza na kasi nayo, inajumuisha kuimarisha yaliyotangulia, ikiwa hatua anayoichukua kwa staili ya maboresho ya ndani ya nchi na uhusiano kimataifa, mambo ambayo yanatoa majibu ya haraka.




Rais Samia Suluhu Hassan, siku alipokabidhiwa tuzo na Benki ya Afrika jijini Accra, Ghana hivi karibuni.

**AKIWA BUNGENI**

Katika hotuba yake bungeni mwaka jana, Rais Samia alifafanua kwa sura pana nchi ilikosimama na inakoelekea, akisema ni mafanikio na wakati huohuo kuna jitihada zaidi zinahitajika kukuza uchumi na kupambana na umasikini nchini.

Rais Samia akarejea nadharia ya wataalamu wa uchumi kwamba, 'ili kupambana na umasikini, uchumi unatakiwa

kukua kwa wastani wa asilimia nane kwa mwaka'. Hata hivyo, kutokana na pigo kimataifa la janga la ugonjwa corona, uchumi wa sehemu nyingi duniani umeshuka kwa kiwango asilimia 6.9 hadi asilimia 4.7.

**HAPO ANAFAFANUA:**

"Hii inamaanisha kwamba, katika miaka mitano ijayo kunahitajika uwekezaji mkubwa katika sekta za uzalishaji na zitazotoa ajira

kwa wingi."

Anatamka mafanikio kwamba Tanzania imepunguza umasikini hadi mwaka juzi ikaingia kwenye Kundi la Nchi za Uchumi wa Kati, pato la wastani wa kila Mtanzania kuongezeka hadi kufikia Dola za Marekani 1,080, zaidi ya kigezo cha Dola za Marekani 1,036 cha kuingia kwenye kundi hilo.

**ZIARA KIMATAIFA**

Katika hatua yake ambayo daima hajaiweka kando diplomasia kimataifa, ameshazuru nchi za barani Afrika; Rwanda, Kenya, Ethiopia, Burundi, Uganda, Afrika Kusini, Namibia, Malawi na Zimbabwe akiweka sawa uchumi wa Tanzania kwa biashara na uwekezaji.

Hapo kukashuhudiwa kuwa miongoni mwa matokeo yake chanya yakijumuisha kufunguliwa fursa za kibiashara nchini Kenya, huku kukiwapo uhusiano na mashauriano bora ya kiuchumi na Uganda.

Pia, katika safari za kufungua milango ya uchumi barani Ulaya, ikamchukua zaidi ya wiki moja katika nchi za Ufaransa na Ubelgiji, hata aliporejea akakiri imefungua hata milango ya uhusiano kijamii

Ni ziara inayotajwa kuleta nchini fedha za msaada kiasi cha Euro milioni 450 au sawa na Shilingi trilioni1.17 kutoka Umoja wa Ulaya (EU), ikiwa ni sehemu ya Euro bilioni 55 zilizotengwa na umoja huo kwa ajili ya Afrika kukabiliana na janga la Covid 19, nako kukishuhudiwa matokeo chanya katika miradi ya maendeleo ya jamii kitaifa.

Rais Samia, pia hivi karibuni akasonga nchini Marekani, ikiwa mahsusi kwa sinema ya aina yake kuibeba sekta za utalii na maliasili nchini, ambayo sasa ni gumzo la dunia. Zao lake kunashuhudiwa mlolongo wa watalii na wakala wao kutua nchini, kupitia mvuto huo baada ya kuzinduliwa.

Akiwa nchini Marekani, Rais akawa na mazungumzo na Makamu Rais wa Marekani, Kamala Haris, kwa lengo la kufufua sekta ya utalii nchini Tanzania na kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo mbili.

Kabla ya kufanya mazungumzo katika jengo la ofisi ya serikali la Eisenhower mjini Washington karibu na Ikulu ya White House, Makamu wa Rais wa Marekani Kamala Haris alibainisha wazi ajenda akitamka:

"Ziara ya Rais wa Tanzania nchini Marekani, inatoa mwanya kwa Marekani kutafuta fursa za uwekezaji kwa kuzingatia kwamba suala hilo lina uhusiano na uchumi kwa ujumla, pia katika sekta ya utalii."

Rais Samia akiwa na mwenyeji wake, Makamu wa Rais Kamala, kukafafanuliwa kuwa ni ziara inayohamasisha uwekezaji mpya wa karibu dola bilioni moja kutoka kwa kampuni mbalimbali za Marekani.

Hiyo inaelezwa ni ziara inayochangia katika ukuaji uchumi nchini Tanzania na wakati huo huo inasaidia kukuza uchumi na kuongeza ajira huko Marekani, Rais Samia akisisitiza haja ya kuwepo ushirikiano wa karibu na sekta binafsi nchini Tanzania,

Anasema, taifa tayari limeshaweka mazingira mazuri ili kustawisha sekta hiyo, akinukuliwa na vyombo vya habari na tamko lake ni: "Ombi langu (Rais Samia) la pekee hapa ni kuitaka serikali ya Marekani kuhimiza zaidi sekta binafsi kufanya kazi nasi."

**JICHO LA WIZARANI**

Katika uwasilisho wake wa makadirio ya Waziri ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji mwaka huu, uwekezaji viwandani umeendelea kukua na kumilikiwa kwa sehemu

kubwa na sekta binafsi na viwanda vingi, vinajishughulisha na uongezaji thamani kwa kutumia malighafi za ndani.

Aidha, anasema sehemu kubwa ya viwanda hivyo ni vidogo sana ambavyo ni 62,400 (asilimia 77.07); vidogo ni 17,267 (asilimia 21.33); vya kati 684 (asilimia 0.84); na vikubwa ni 618 (asilimia 0.76).

Pia, mchumi Dk. Kijaji anasema usajili wa viwanda chini ya Kituo cha Uwekezaji (TIC) na EPZA, inategemewa kuwa na viwanda vipya vikubwa 500 vitajengwa katika miaka mitano ijayo, hadi kufika mwaka 2025,

Hapo anasema, idadi ya sasa ya viwanda vikubwa vinavyoajiri wafanyakazi zaidi ya 500, imeongezeka kutoka 41 hadi 541.

Anafafanua: "Serikali ya Awamu ya Sita imeanza utekelezaji wa Kongani ya Viwanda ya Kwala ambayo uwekezaji wake ni takriban Dola za Marekani bilioni tatu ambayo itakuwa na viwanda 200 vikubwa kwa ajili ya kutengeneza nguo, vifaa vya umeme, vifaa vya ujenzi, dawa na aina nyingine. Awamu ya kwanza itakamilika mwaka 2024 na kutoa ajira za moja kwa moja 100,000 na zisizo za moja kwa moja 300,000."

"Serikali ikishirikiana na sekta binafsi itajenga viwanda katika maeneo maalum ya Nala - Dodoma na kongani itakayojengwa katika mkoa wa Mwanza. Uwekezaji huo utachochea matumizi ya reli ya kisasa ya SGR, bandari za Maziwa Makuu, bahari pamoja na barabara. Uwekezaji huo utaifanya Tanzania kuwa nguzo ya uchumi ya Bara la Afrika (Africa Economic Power House) na kiunganishi kupitia Bahari - GateWay."

**BIASHARA KIMATAIFA**

Waziri anasema, soko la China limeongezeka kwa asilimia 14.31 na kufikia Dola za Marekani milioni 273.1 kwa mwaka 2021, kutokana na uzalishaji na uuzaji kwa wingi hususan tumbaku, pamba na mbegu za ufuta.

Pia, anasema soko la India, limeongezeka kwa asilimia 90.79 na kufikia wastani wa Dola za Marekani bilioni moja (Dola milioni1.008) mwaka 2021, kulikotokana na ongezeko la mauzo ya madini, pia mazao ya kilimo korosho, mbaazi na maharage ya soya.

Anataja mauzo katika soko la Japan yaliongezeka kwa asilimia 20.97 na kufikia Dola za Marekani milioni 67.5 mwaka 2021 na Mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Jumuiya ya Ulaya (EU) yalipungua kwa asilimia 41.89.

"Aidha, mauzo ya Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2021 yaliongezeka kwa asilimia 43.73 na kufikia Dola za Marekani Milioni 1,161.2 mwaka 2021 kutokana na ongezeko la mauzo ya chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, bidhaa za karatasi, mabati, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), saruji na mafuta ya kupaka," anaeleza na kuongeza:

"Mauzo ya Tanzania kwenda katika soko la nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini (SADC) mwa Afrika yalipungua kwa asilimia 10.06 kufikia Dola za Marekani milioni 1,311.5 mwaka 2021."

Wakati Waziri Dk. Kijaji, akifafanua bungeni upandaji bei usioendana na uhalisia katika soko kwa baadhi ya bidhaa hasa zinazoagizwa kutoka nje, katika kipindi cha kuanzia mwezi Desemba mwaka jana, akitoa mfano wa bidhaa za ujenzi, vyakula, nishati na pembejeo za kilimo, serikali ilishatolea ufafanuzi wa hatua zake.

Ni hatua zinazoendeshwa,huku nyingine endelevu zikidumishwa kama vile za ujenzi mbalimbali, ikiwamo reli ya kisasa (SGR), mradi wa umeme wa Mwalimu Nyerere,

pia, kuna miradi ya gesi iliyofafanuliwa juzi bungeni na Waziri wa Nishati, January Makamba na hatua za udhibiti wa bei ya mafuta ambayo inazua taharuki kimataifa.

Katika taswira hiyo, hivi karibuni Rais Samia alipozindua miradi ya barabara mkoani Tabora, siku chache baadaye akapata tuzo ya kimataifa kutoka Benki ya Afrika huko jijini Accra, Ghana, akiwekeza pia kwa wafanyabiashara wadogo Machinga, akiwaahidi mengi ikiwamo ofisi mpya kila mkoa.


Hali kadhalika, katika uwekezaji wa utumishi serikalini kupata ongezeko la mishahara na madaraka yao ya vyeo kufanyiwa kazi, jana Rais Samia akakubali kuwa mlezi wa Chama cha Makatibu Mahsusi, ambao ni mwendelezo wa uwekezaji katika sura ya utumishi wenye tija.



Rais Samia Suluhu Hassan, alipoingia bungeni jijini Dodoma, kwenda kuhutubia. **PICHA: MTANDAO.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Watanzania tulipie elimu au matibabu?






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

TANZANIA ni mahali pazuri sana pa mtu kuishi, kwani ndipo unaweza kusikia hoja inaibuliwa na kujadiliwa kwa nguvu kubwa, na kisha kufa kifo cha mende na kusubiri kipindi kingine cha mwaka kuwadia.

Hivi sasa katika kipindi hiki cha mkutano wa Bunge la Bajeti,

ndipo utasikia masuala mbalimbali yakijadiliwa kwa nguvu kubwa na ubishani mkali baina ya wabunge na mawaziri, yaani wananchi na serikali yao. Lakini, mkutano huu utakapomalizika na kila mtu kurudi anakostahili kuwa, yote yanakuwa kimya na inaibuka hoja nyingine mitandaoni, inayotawala mawazo ya Watanzania hawa na kusahau hata umasikini wao.

Nimekuwa mmoja wa wenye kiherehere cha kusikia nini kinajadiliwa bungeni na wawakilishi wetu na kujibiwa na mawaziri. Yapo yanayovutia na kufurahisha, lakini mengine ni ukakasi.

Hata hivyo, hunipa kianzio cha name kushughulisha akili yangu ambayo pengine inaweza isivuke mipaka na kubakia kwangu na kusaidia kidogo familia niliyojitengenezea kwa makusudi.

Nimekuwa mara kwa mara nikipenda sana kusikiliza hoja kuhusu huduma za jamii, hususan za elimu na afya. Ndiyo sababu hupenda sana kumsikiliza Mbunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba, maarufu Profesa.

Mbunge huyo hukaa kimya akisikiliza wengine, lakini anapopewa fursa ya kusimama kuzungumza, kila mmoja hujikuta akihoji halmashauri ya kichwa chake, kama alisikia vizuri na kuamua kuzingatia au la, kutokana wa staili ya anachowasilisha.

Mimi huzingatia sana maneno yake yanayolenga kuangalia mustakabali wa elimu nchini, kama inawasaidia wanetu katika kujikomboa wao na kutukomboa sisi wazazi wao, lakini Taifa kwa ujumla.

Hatimaye ukimsikiliza vizuri Kishimba, utaona elimu tunayopeana hapa nchini, haina tofauti na kutwanga maji kwenye kinu, tunaishia kujilowanisha tu wenyewe bila kunufaika na chochote.

Hiyo inaonyesha ni jinsi gani hatujipangi tukawa na dira au mwelekeo unaoeleweka utakaotupa tija katika elimu tunayopeana, licha ya kuwa na mikutano ya Bunge kila mwaka.

Hoja yake, ni kwamba tunapeleka wanetu shuleni wanasoma na kuhitimu, lakini hatimaye wanarudi majumbani kukaa kama walivyokuwa kabla hawajaanza shule. Maana yake tunapoteza muda kusoma na kusomesha.

Ukitafakari sana na ukaona vijana wangapi waliohitimu elimu zao na kuoanisha na wanachokifanya sasa, huku wakubwa wakiwahimiza kujiajiri kana kwamba shuleni walifundishwa kujiajiri, utashangaa.

Hapo ndipo nami nakuja na mawazo yangu na kujiuliza kama kati ya elimu na afya nini kinatakiwa kutolewa bure kwa watu, najikuta natetea afya iwe bure kuliko elimu.

Wazo hilo halinifanyi kupinga sera ya Dk. John Magufuli (alazwe pema) ya elimu bila malipo, ingawa kuna vijimalipo vinafanywa na baadhi ya shule, lakini kama hakuna faida hata ukisoma bure ukarudi nyumbani, ndiyo nini?

Watu husema bila elimu huwezi kumpata daktari anayekutibu, lakini elimu ya leo hii ina maana gani, kama hata hao madaktari wanamaliza, lakini wakarudi mitaani kutafuta ajira na kuambiwa jiajirini?

Pia, kama sifa ya kuwa mbunge mpaka leo ni kujua kusoma na kuandika, kuna sababu gani ya mtoto kuzeekea shuleni na vyuoni na kurudi nyumbani kuungana na wazazi wake, kwa kukosa mahali pa kwenda kutumikia alichosoma?

Ukikosa elimu si rahisi kufa, lakini ukikosa huduma ya afya ni rahisi kufa. Tunajua wengi wetu ni masikini, sasa je tujiulize hicho kipato tunachokipata kutokana na juhudi binafsi, tukipeleke shuleni au hospitalini?

Kwa akili hii ninayotumia kuandika hapa, mimi ningependekeza shuleni tujilipie, lakini hospitalini tulipiwe. Yaani ile pesa inayotolewa kila mwezi shuleni chini ya sera ya elimu bila malipo, iende hospitalini kwa sera ya tiba bila malipo.

Hiyo itafanya watu wasiendelee kusumbuliwa na maradhi ambayo si rahisi mtu kupambana nayo, kuliko kupambana na ujinga ambao unaweza kuondoka hata kwa watu kueleweshana tu hiki kibaya na hiki kizuri, na si ugonjwa. Kwa sababu naona hili la bima ya afya ni kizungumkuti. Alamsiki!

BIASHARA

# Unataka kukopa au kukopesha? Pata siasa zake kutoka wataaluma wa fani

## •Dondoo za Ustadh, Mchungaji....

**Na Maira Blyden, SJMC**

SUALA la kukopa na kukopeshana ni kawaida kwa wanajamii hususan za Kiafrika, ikiwa ni njia ya kusaidiana penye uhitaji na ndiyo sehemu ya utamaduni wa kufanikisha maisha, hata kufikia malengo au hatua binafsi.

Mkopo unaweza kuwa wa pesa au vifaa, ambavyo mtu hupewa kufanikisha alichokinuia. Mkopo unaweza kuwa wenye riba au la, kulingana na makubaliano baina ya mkopeshaji na anayekopeshwa.

Zipo taasisi nyingi rasmi zinazotoa mikopo ya riba. Pia, kuna njia ya pili, watu wanakopeshana kwa njia zisizo rasmi, pia kirafiki au kindugu na kimsingi kukopesha ndiyo biashara kuu ya taasisi za fedha.

Hapo penye urafiki, dhamana kuu huanzia kwenye uaminifu wa anayepewa. Ni bahati mbaya kanuni hiyo inapuuzwa sana na wengi na ndio mwanzo wa kutorejeshwa madeni kabisa au kwa wakati.

Mzee Mukota Chikombe, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) anayefanya biashara zake mjini Dar es Salaam, ana simulizi iliyobeba uzoefu wake binafsi.

"Kuna kaka yangu aliwahi kunikopa fedha akafanye biashara kwa makubaliano kwamba atanirejeshea baada ya mwezi, lakini hakufanya hivyo. Akanigeuka, akawa mkaidi sana ndipo nikaamua kuwaita ndugu nikawaeleza lakini haikusaidia, si unajua mambo ya undugu wakasema nimsamehe na yaishe!" anasimulia.

Mzee Chikombe anasimulia aliamua kuepusha rabsha itokanayo na hilo, akiendeleza simulizi kwamba: "Kutokana na jinsi ndugu yangu alivyonitendea kwa kunidhulumu pesa yangu. Naona ni heri ukamsaidia mtu baki, maana ndugu wamekuwa si waaminifu na iwapo umeamua kumsaidia mpe kiasi kidogo ambacho hata asipokurudishia hautaumia."

Hayo yanajiri, huku kukiwapo usemi mkongwe "Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli". Inaelezwa, kutokuzingatia hali wanazopitia wadeni nao kuna nafasi yake, ikifafanuliwa, ni hali inayoleta sintofahamu na wengine wanashindwa kulipa kwa wakati, kutokana na kutokuwa



Shughuli za kibiashara zikiendelea, ambazo kwa kiasi kikubwa zina unasaba na mikopo. **PICHA: MTANDAO**

vizuri kifedha kwa wakati husika.

Mawasiliano ni nyenzo muhimu sana maishani iwe katika uwasilishaji wa hali, hisia na hata mitizamo na yanapokuwa dhaifu, huvuruga uhusiano baina ya mkopaji na mkopeshaji.

"Kibinadamu ukikopa halafu muda wa kurejesha ukifika na hauna kitu cha kurejesha basi toa taarifa kwa mdeni wako ili aelewe kinachoendelea, kukaa kimya inaonyesha hujali chochote, hivyo ni lazima mtofautiane," anasema Grenvin Ngede, mkazi wa Makumbusho Kijitonyama, Dar .

Wanajamii wanasema, moja ya sababu kuu ya wadeni kuhitilafiana ni namna inayotumiwa na mkopaji kumdai mdeni, lugha isiyofaa ya kejeli na matusi mara nyingi huibua hisia za chuki kwa mdaiwa kiasi cha wengine kuamua kutolipa kwa makusudi, kumkomoa mdai.

"Watu wengine sio wastaarabu, wanapokopeshwa, ukimfuata kwa upole ataanza kukupelekesha, na kwamba pesa hiyo iliyomsaidia angeweza kupata hata kwa mwingine, jibu kama hilo linatia hasira," anasimulia Magreth Tweve, mkazi wa Mikocheni Dar es Salaam, na anaendelea: "Wakati mwingine tutizame watu tunaowakopesha."

"Pasi na kutumia ukali pengine inawezekana isiwe rahisi mtu kukuelewa hasa wale wanaongojea mpaka wasukumwe ndipo warejeshe, japo pia si vyema kutumia maneno ya vitisho ambayo yatakutia matatani akiamua kukushtaki,"anafahamisha Benson Sombe, mkazi wa Tandale, Dar es Salaam .

Mwingine, Aisha Mbuma, Mkazi wa Kijitonyama, Dar es Salaam, ana mchango wake: "Unaweza kutumia lugha nzuri ya upole mdeni wako akakuchukulia kuwa wewe ni mdhaifu akakudharau, pia unaweza kuongea naye kwa lugha ya ukali na yeye akaona awe mkaidi, akasema silipi, ikawa kama vita sasa."

"Huwezi kwenda kumdai mtu mbele za watu tena kwa kumfokea, unamdhalilisha, ni haki yako ndio lakini haipendezi," anaunga mkono Mzee Kilaghinja Mziray, Mkazi wa Mwenge, Dar es Salaam.

### TAFSIRI YA MKOPO

Kimsingi, inafafanuliwa mtu anapomkopesha mwingime fedha, ni ishara kubwa na pandikizi la uaminifu kwa anayekopeshwa na malipo yake ni fadhila, wala si vinginevyo.

Siku zote inaelezwa kuwa uaminifu hupimwa kwa mambo machache, huku Mchungaji Paulo Bendera, Askofu Mkuu wa Makanisa ya Ufunuo Tanzania, akieleza maandiko matakatifu yanaendana na sheria za nchi, hairuhusu kumdhulumu mtu na ndio maana sheria huwatia hatiani wanaoenda kinyume nayo.

Mchungaji Bendera, anasisitiza watu wasidharau kwamba hiyo ni fedha kidogo, lakini huchachua mfumo mkubwa wa maisha, akiwa na ufafanuzi:

"Unaweza kuiona nyumba uliyokabidhiwa ni ya thamani kubwa kuliko shilingi elfu moja, kwa kushindwa kufikiria ya kuwa huenda hiyo elfu moja ndio kiasi pekee yule aliyekukopesha alikuwa nacho. Hivyo, kudharau vidogo ni dhambi.

"Dini imetilia mkazo juu ya kumkabidhi mtu amana iwe ndogo au kubwa, kwa kigezo cha kuwepo maandishi ya makubaliano au rehani (Kitu unachotakiwa kumpa anayekukopesha ili akuamini)," anasema Shekhe Juma Farijala, kutoka msikiti ulioko Ukonga, akiikumbusha jamii katika somo nyeti la uaminifu.

"Wanajamii waache hiyana na ikitokea mtu kakudhulumu na hamkuandikishana yafaa unuie sadaka. Si vyema kumuombea mtu dua mbaya, badala yake muombee kwa Mwenyezi Mungu ili arudi kwenye haki," anaeleza. Shekhe Farijala.

Mtazamo wa hoja yake, inafafanuliwa zaidi na Mchungaji Bendera, kwamba:"Fedha ya kukopa huwezi irejesha kama huna msingi."

Anaendelea: "Ni vizuri kuwa na msingi au chanzo kitakachosaidia kurejesha mkopo uliopewa kwa wakati, jambo litakalokujengea uaminifu siku nyingine utakapokuwa na uhitaji."

Mwanasaikolojia na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Physical and Spiritual Counseling Consultants yenye makao makuu yake Dar es Salaam, Dk. Mkumbo Mitula, anasema anayedaiwa siku zote hupokea shinikizo kutoka kwa anayemdai.

"Anayekopesha ikitokea hajarejeshewa deni lake hukata tamaa, hurudi nyuma kimaendeleo kutokana na morali kushuka hasa ikitokea fedha husika aliipangia malengo fulani, pia ushirikiano wake na jamii hushuka na kusababisha 'umimi' kwa kuwa hatakuwa na imani tena na yeyote.

"Moja ya matatizo waliyonayo wakopeshaji ni kutokuangalia uwezo wa yule anayemkopesha kulipa, kigezo kinachotumika mara nyingi ni undugu, urafiki na ujamaa.

"Anayekopeshwa siku zote deni humfanya kuwa mtumwa, mnyonge hata utu wake pia hupotea. Hali hiyo humuathiri kisaikolojia na kumfanya kuwa na mawazo ya hofu wakati ambao shinikizo toka kwa anayemdai linazidi ilhali hana chochote cha kurejesha,"anaeleza mwanasaikolojia Dk. Mkumbo.



## Watumishi wakiuka maadili kuchukuliwa hatua

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, amewaonya watumishi idara ya ununuzi wanaokiuka maadili kufanya manunuzi watachukuliwa hatua za kisheria.

Chande alisema hayo wakati wa uzinduzi wa kanuni za maadili kwa watumishi wa umma na wazabuni wanaoshiriki katika shughuli za ununuzi wa umma uliofanyika jijini hapo.

Aliwaonya baadhi ya watumishi wa manunuzi ya umma kuacha tabia ya ukiukwaji wa maadili kufanya manunuzi kwa sababu wanaisababishia serikali hasara kutokana na tabia hiyo.

"Serikali itaendelea kuchukulia hatua kali kwa watumishi wale watakaokiuka sheria na kanuni katika manunuzi ya umma," alisema.

Alibainisha kuwa watu wa manunuzi wakikiuka sheria wanaisababishia serikali hasara kubwa kutokana na makubaliano yasiyozingatia sheria.

Kadhalika, alisema serikali inawategemea idara ya manunuzi kwa sababu kwa asilimia kubwa ya fedha za serikali zinapitia kwao.

Naye Kamishna wa Sera na Manunuzi ya Umma Wizara ya Fedha na Mipango, Fedrick Mwakibinga, alisema kanuni hizo zilizozinduliwa jana ni mwongozo kwa ajili ya manunuzi yote ya umma.

Aliyataja malengo mengine ya kutungwa kwa kanuni hizo kuwa ni kuwadhibiti watumishi wasio waaminifu katika manunuzi.

Mwakibinga alisema kutungwa kwa kanununi hizo ilitokana na matatizo yaliyoonekana kwenye manununuzi ya umma na wizara ikaamua ya kutunga kanuni hizo.

Aliyataja matatizo hayo kuwa ni usimamizi mbovu katika manunuzi, uelewa mdogo wa wadau na kuingiliwa kwa ufuatiliaji wa idara.

Aidha, aliwaomba waajiri kuhakikisha wanawaajiri watumishi wenye sifa katika manunuzi ya umma ili kuepuka kuingia kwenye hatia.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema kanuni hizo zitawahusu watu wa manunuzi na watoa huduma wote.

Tutuba, alisema uzinduzi huo umewashirikisha idara zote za manunuzi ya umma pamoja na wadau wengine wa sekta hiyo.

Alibainisha kuwa lengo la kuwashirikisha wadau ni kuwajengea uelewa baada ya kuwa na sera ya manunuzi bila uwapo wa kanuni.

# Bei elekezi matumizi maji vijijini zaja

**Paul Mabeja na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema inaandaa bei elekezi za maji zitakazoanza kutumika maeneo ya vijijini ili kuwezesha kila Mtanzania kupata huduma hiyo kwa bei nafuu na kunufaika na kazi nzuri inayofanywa na serikali ya awamu ya sita.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji pamoja na kumpongeza Rais Samia kwa kuipatia wizara hiyo zaidi ya asilimia 95 ya fedha ilizoomba katika bajeti yake.

Alisema serikali inapanga kuandaa bei elekezi za maji ambazo zitasaidia kuondoa kero ya gharama kubwa katika maeneo ya vijijini.

"Ndoo ya maji maeneo ya vijijini ni Sh. 50 wakati mjini kama pale Dar es Saalam, mtu analipa uniti moja ya maji kwa Sh. 1,500, lakini ukipiga kwa bei ya Sh. 50 ya mtu wa kijiji unapata Sh. 2,500 kwa uniti moja hivyo hii inamaanisha kuwa mtu wa mjini pale Dar analipa ndoo moja ya maji kwa Sh. 30.

"Hivyo tunapanga kuleta bei elekezi hizi ambazo zitakwenda kuondoa kero hii na bei hizi zitaonyesha kuwa mtu ambaye anachota maji katika chanzo kinachoendeshwa kwa umeme ni bei gani, chanzo kinachotumia sola bei gani, lakini kinachotumia mafuta bei gani ili kuondoa adha na kila mtu afurahie bei rahisi na nafuu za maji na kunufaika na kazi nzuri inayofanywa na serikali ya awamu ya sita," alisema Aweso.

Alisema wizara yake itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji ili kuhakikisha kuwa huduma ya majisafi na salama na yakutosheleza yanapatikana katika maeneo yote ya mijini na vijijini.

Kadhalika, aliwaagiza wataalamu wa manunuzi kuanza kufanya michakato ya kuwapata makandarasi mapema ili miradi ya maji ikamilike kwa muda mfupi.

"Azma ya Rais wetu ya kumtua mama ndoo kichwani ni jambo la lazima michakato ya manunuzi ianze sasa sio mnasubiri hadi mwezi Novemba, hatuna sababu ya miradi ya maji kutumia muda mrefu kukamilika awamu hii tunakwenda kutekeleza miradi 175 ya maji mijini na vijijini ni miradi 1,163," alisema Aweso.

Vilevile, alisema makandarasi watakaotekeleza miradi ya maji wanatakiwa kupatikana wenye uwezo na serikali haitakuwa kikwazo cha kuchelewesha malipo yao.

"Aidha, naagiza kuwa mteja atakayelipia huduma ya kuunganishiwa maji apatiwe huduma hiyo ndani ya siku saba na sio vinginevyo na sisi kama wizara tunajipanga kusimamia na kufuatilia upatikanaji wa huduma za maji," alisisitiza.



Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC) Dk. Franklin Rwezimula (katikati), akishiriki zoezi la upandaji miti katika Chuo cha Mipango Dodoma juzi, ikiwa ni sehemu ya Wiki ya Mazingira. Wengine ni mabalozi wa mazingira, Sakina Abdulmasoud (kushoto) na Oliver Nyeriga. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

# Jafo asisitiza uzingatiaji utunzaji mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ametaka wananchi kuzingatia uhifadhi na utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari za kiuchumi.

Akizungumza juzi na wanafunzi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini baada ya kujionea jitihada za wadau wa upandaji miti na usafi wa mazingira ikiwa ni sehemu ya Wiki ya Mazingira, Waziri Jafo alisema ukame ukishamiri husababisha uzalishaji kuwa mdogo kwa kuwa zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania wategemea kilimo.

"Ukame ukishamiri uzalishaji kwenye kilimo unakuwa mdogo, asilimia 29.2 ya Pato la Taifa linatokana na kilimo, zaidi ya asilimia 32 ya usafirishaji nje ya nchi unatokana na kilimo, ukame ukishamiri na kilimo kikawa kidogo uchumi wetu utakuwa hatarini," alisema. Alihimiza upandaji miti kwa wanafunzi na kuhifadhi mazingira kwa kuwa wataalamu wanasema asilimia 62 ya miti inayopandwa inakuwa himilivu.

Akitoa tamko la Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC) kuelekea kilele cha Siku ya Mazingira Duniani, Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, Dk. Franklin Rwezimula, aliwaasa wanafunzi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP), kujiunga kwenye programu ya wataalamu elekezi ili wajiajiri wenyewe na kufanya shughuli za maandiko na tathmini ya mazingira.

Alisema kwa sasa Tanzania inakabiliwa na uhaba wa wataalamu wa kuandika tathmini ya mazingira na wanaamini chuo hicho kitatoa wataalamu wengi watakaosaidia kupunguza pengo lililoko la wataalamu hao nchini.

"Chuo cha Mipango ni wadau wakubwa wa mazingira kwa kuwa wanafundisha wataalamu wa mazingira na kufanya ushauri wa masuala ya mazingira, tathmini ya athari za mazingira, NEMC na Chuo cha Mipango tumekuwa tukishirikiana nao kwa namna mbalimbali ambapo tunapokea wanafunzi wanaokuja kujifunza mafunzo kwa vitendo na tunawafundisha kazi ya NEMC, tunashirikiana na walimu katika kufanya tafiti mbalimbali," alisema.

Naye mmoja wa wanafunzi mwanachama wa klabu ya mazingira ya chuo hicho, Modesta Yohana, alisema klabu yao imekuwa ikipanda miti na kutengeneza bustani ili kukijanisha chuo hicho.

Alisema wamekuwa wakienda maeneo mbalimbali jirani na chuo kuhamasisha wananchi kupanda miti, ili kukabiliana na athari za mazingira zilizoko.

"Wito wangu kwa wananchi waweke juhudi katika kupanda miti na kutunza mazingira yetu kwa ajili ya kizazi kijacho," alisema.



# Watembea kilomita 200 kupata huduma za uzazi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANAWAKE wanaoishi Kata ya Kambikatoto wilayani Chunya, Mbeya, wanalazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita 200 kwenda kujifungua au kupata huduma zingine za afya katika Hospitali ya Wilaya iliyoko Chunya mjini.

Pia baadhi ya wanawake husafiri kwenda katika Hospitali ya Itigi iliyoko mkoani Singinda ambayo nayo iko umbali wa kilomita 200 kutoka kwenye makazi yao kwa ajili ya huduma za uzazi.

Sambamba na hiyo, imeelezwa kuwa wale ambao hawana uwezo wa kifedha hujifungulia nyumbani au kwa waganga wa tiba za asili.

Hali hiyo inatokana na eneo hilo kutokuwa na vituo vya kutolea huduma za afya tangu nchi ilipopata uhuru mwaka 1961.

Waliyasema hayo wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilipofanya ziara kukagua ujenzi wa kituo cha afya ambacho kinajengwa na serikali kwa kushirikiana na wananchi wa kata hiyo kwa zaidi ya Sh. milioni 250.

Mmoja wa wanawake hao, Sarah Bahati, alisema pamoja na kwamba wanakopata huduma hizo ni mbali, pia kuna tatizo la miundombinu ya barabara kuwa mibovu hali inayowafanya wateseke wakati wa kusafiri.

Alisema wanapotaka kusafiri kwenda Chunya wanategemea usafiri wa mabasi yanayotoka mkoani Tabora ambayo huwa yanapita mara moja kila siku na kwamba likishaondoka wanashindwa kusafiri, hivyo kupata maumivu zaidi.

Aliishukuru serikali kwa kuamua kuwajengea kituo cha afya katika eneo hilo kwamba kitawapunguzia adha ya kusafiri siku zote, hivyo huduma zote watakuwa wanazipata jirani na makazi yao.

"Hii itatupunguzia gharama za usafiri na hivyo tutazitumia fedha ambazo tunazitafuta kwa ajili ya kujihudumia kwa mambo mengine kama kununua nguo na chakula baada ya kujifungua," alisema Sarah.

Alisema baadhi ya wanawake walikuwa wanafariki njiani na wengine kujifungulia njiani kutokana na kuchelewa kufika hospitalini na kwamba hali hiyo ilikuwa inahatarisha maisha yao.

Naye Vumilia Modest alisema wanawake wengi walikuwa wanapata wasiwasi baada ya kupata ujauzito wakihofia usafiri wa kwenda kupata huduma hospitalini.

Alisema kwa sasa wameanza kupata amani kutokana na mradi wa ujenzi wa kituo cha afya ambao unaelekea kukamilika na hivi karibuni utafunguliwa huku akisisitiza kuwa jengo la mama na mtoto litakapokamilika litawasaidia.

Alisema kwenye usafiri wa umma waliokuwa wanautumia wakati wa kwenda kujifungua ulikuwa unakuwa kero kwao na kwa abiria wengine wanaoutumia.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, alisema amekuwa akitembelea kituo hicho mara kwa mara ili kuhakikisha kinakamilika kwa wakati na wananchi wanaanza kupata huduma.

Alisema mbali na fedha ambazo zilipelekwa na serikali pia wananchi wamechangia nguvu zao ambazo zikithaminishwa na fedha ni sawa na zaidi ya Sh. Milioni 30.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homela aliagiza kituo hicho kianze kufanya kazi Juni 30 huku akiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuhakikisha inachimba kisima kwa ajili ya maji yatakayokuwa yanatumika.

Pia aliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha umeme unapofika katika eneo hilo kipaombele cha kwanza iwe kwenye Kituo cha Afya na kwenye makazi ya wananchi.




Balozi wa Biko Tanzania, Kajala Masanja (kushoto), akikabidhi zawadi ya Sh. Milioni 10 kwa mshindi wa droo kubwa ya bahati nasibu ya Biko, Aziza Selemani, katika benki ya CRDB, Tawi la Premier, Palm Beach, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wahadharishwa wahamiaji haramu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewataka wananchi wilayani hapa kutoa ushirikiano ili kudhibiti wahamiaji haramu ambao kwa sasa wameanza kupita wakitokea Tabora baada ya ulinzi kuimarishwa zaidi kwenye barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, aliyasema hayo juzi baada ya wahamiaji haramu 40 kunaswa wakisafirishwa kwenda Mbeya wakipitia katika njia hiyo.

Alisema kwa sasa baada ya barabara ya Mbeya-Tabora kuboreshwa, wasafirishaji wa wahamiaji haramu wameanza kupita huko wakikwepa kunaswa kwenye maeneo mengine ambayo ulinzi umeimarishwa.

Kamanda Matei alisema wahamiaji haramu wanaopita mara nyingi ni wa Ethiopia na kwamba hata waliokamatwa hivi karibuni walikuwa raia wa nchi hiyo na walipowahoji walisema walikuwa wanakwenda Malawi na kisha Afrika Kusini.

Alisema baadhi ya wasafirishaji wa wahamiaji haramu hao wamekuwa wakitumia magari ya mizigo na hata magari madogo na hivyo akawataka wananchi kusaidia kutoa taarifa kwenye mamlaka ili wakamatwe.

"Ukimuona mtu ambaye humfahamu na hujui amekuja kufanya nini, ni vizuri ukatoa taarifa kwa viongozi ili mtu huyo achunguzwe. Hii njia baada ya kuboreshwa wasafirishaji wa wahamiaji haramu wameanza kuitumia," alisema Kamanda Matei.

Alisema kwa mujibu wa sheria, mtu yeyote anayebainika kufanya kazi ya kusafirisha wahamiaji haramu anafanya kosa la jinai ambalo linaweza kumsababishia matatizo, hivyo akawataka wahusika kuacha tabia hiyo.

Gari lolote, alisema linalokamatwa likisafirisha wahamiaji haramu linataifishwa na mhusika kupelekwa mahakamani na akipatikana na hatia anapelekwa gerezani na kwamba faini yake ni kubwa.

Ofisa Uhamiaji wa Wilaya ya Chunya, Mrakibu Msaidizi wa Uhamiaji Venance Luwagila, alisema mara nyingi wasafirishaji wa wahamiaji hao wanatumia magari ya mizigo na madogo pamoja na pikipiki.

Alisema baadhi wamekuwa wakisafirishwa kwenye magari yanayokuwa yanasafirisha machungwa ambapo wahamiaji hao hufichwa kwenye machungwa na kufunikwa na maturubai.

Alisema baada ya kubaini hali hiyo waliamua kuongeza umakini kwenye maeneo ya vizuizi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha magari yote yanayopita yanakaguliwa ili kujua watu ambao wanakuwa wamebebwa humo.

## Wafurahia kurejeshwa maonyesho ya Nanenane

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADA ya serikali kutangaza kuwa maonyesho ya wakulima, maarufu kwa jina la Nenenane yatafanyika mkoani Mbeya, baadhi ya wananchi wamesema hafla hiyo ni fursa kwao kiuchumi.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wananchi walisema watayatumia maonyesho hayo kupata elimu ya kilimo na ufugaji lakini kutokana na kukusanya watu wengi itakuwa fursa kibiashara.

Mmoja wa wananchi hao, Julius Nsyukwe, alisema baada ya serikali kutangaza uamuzi huo, wananchi wengi wameanza maandalizi ya shughuli mbalimbali.

Alisema yeye ni mjasiriamali ambaye anafanya shughuli zake za kuuza chips katika soko la Mwanjelwa lakini kipindi cha Nanenane anahamishia shughuli zake katika viwanja vya John Mwakangale ambako ndiko maonyesho hayo hufanyika.

"Maonyesho haya yakifanyika kikanda tumekuwa tukipata fedha nyingi sana, sasa kwa kuwa maonyesho haya yatafanyika kitaifa naamini tutapata fedha nyingi zaidi," alisema Nsyukwe.

Naye Sephania Shororo alisema kwenye maonyesho hayo watajifunza mbinu nyingi za kilimo bora na kwamba zitawasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali na hivyo kuinuka kiuchumi.

Juzi, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitangaza kuwa serikali imerejesha maonyesho ya Nanenane ambayo yalisitishwa mwaka jana kutokana na ugonjwa wa UVIKO- 19 na kwamba kitaifa yatafanyika mkoani Mbeya.



# Boti nane kununuliwa kwa doria baharini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesema inakusudia kununua boti nane ambazo zitatumika kwa ajili ya kufanya doria katika maeneo ya hifadhi ili kupambana na uvuvi haramu unaoharibu matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Suleiman Masoud Makame, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23 katika Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar.

Makame alisema uchumi wa buluu hauwezi kupata mafanikio kama serikali haitoweka kipaumbele katika kudhibiti uvuvi haramu unaofanywa na wavuvi ambao si waaminifu.

Alisema katika ununuzi wa boti hizo, kipaumbele kimewekwa katika kudhibiti maeneo ya uvuvi ambayo yako chini ya hifadhi ya mazingira.

"Mheshimiwa Spika napenda niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tunakusudia kununuwa boti tano zitakazotumika katika kulinda maeneo ya hifadhi ya uvuvi ambayo yametengwa kwa ajili ya kazi hizo," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri, hivi sasa kumejitokeza matukio ya baadhi ya wavuvi kuvamia maeneo ya hifadhi na kuendesha uvuvi kinyume cha sheria.

Alisema wavuvi wamekuwa wakitumia aina ya uvuvi ambao haukubaliki unaoharibu mazingira ya baharini ikiwemo matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki.

Pia alisema baadhi ya wavuvi wanavua samaki katika maeneo yaliyopo chini ya hifadhi kwa kutumia nyavu zenye macho madogo ambazo ni hatari kwa kunasa samaki wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya binadamu.

Waziri huyo alisema ununuzi wa boti kwa kiasi kikubwa unakwenda kulipatia ufumbuzi tatizo la migogoro ya uvuvi inayotokana na uvuvi usiokubalika wenye kuathiri maendeleo ya uvuvi na mazalia ya baharini.

Alikiri katika siku za hivi karibuni kumejitokeza matukio mbalimbali ya wavuvi katika vijiji jirani kugombana kwa kutuhumiana kuendesha uvuvi unaoharibu mazingira ya baharini na mazao ya samaki na matumbawe.

# Othman ataka ujenzi miundombinu wenye maono kukidhi vizazi vijavyo

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni muhimu kwa jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kufikiria matumizi ya muda mrefu ya rasilimali hasa wakati wa ujenzi wa miundombinu.

Amesema katika kufanya hivyo, taasisi zinapaswa kutumia ardhi kwa usahihi hata kama ni ndogo kiasi gani.

Othman aliyasema hayo jana katika Shule ya Mizingani wilaya ya mkoani Pemba, alipokagua ujenzi wa madarasa mapya ya shule hiyo yaliyojengwa kutokana na fedha za ahueni za UVIKO- 19 akiwa katika mwendelezo wa ziara maalum ya kukagua sekta ya elimu.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia kupatikana majengo yanayoweza kusaidia mahitaji yaliyopo na kwenda sambamba na ongezeko la idadi ya watu ambapo mahitaji yao ya upatikanaji wa huduma mbalimbali nayo yanaongezeka kwa kila eneo ikiwamo elimu.

Othman alisema kutokana na hali hiyo, ni vyema kufikiria mbali zaidi wakati wa kuanzisha ujenzi wa majengo ya huduma za elimu na madarasa ya shule sambamba na kuangalia maeneo yanayotumiwa kwa ujenzi kuwa ni yale yasiyofaa kwa shughuli za kilimo.

Pia alibainisha kwamba serikali itaijenga upya na kuwa bora zaidi Shule ya Ufundi Kengeja iliyoungua moto hivi karibuni.

Alisema hivi sasa serikali inaendelea kutathmini gharama zilitokana na ajali hiyo sambamba na kufikiria upya ujenzi utakaokuwa wa kisasa na kukidhi mahitaji mapana zaidi ya baadaye sambamba na uwekaji wa miundombinu bora itakayozuia majanga ya namna hiyo yasitokee kwa urahisi.

Hata hivyo Othman aliwataka wanafunzi kujitahidi kusoma hasa katika fani za masomo ya sayansi na kuachana na vishawishi vya matumizi mabaya ya simu na mitandao ambayo yanaweza kuwaharibia mustakabali wa jitihada zao za kutafuta elimu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Matari Zahoro Masoud, alisema jitihada za serikali zinazoendelea za ujenzi wa majengo mapya ya shule zitasaidia kuondoa changamoto kubwa ya uhaba wa madarasa ya shuleni.

Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Mohammed Nassor, alisema jitihada zinazoendelea za ujenzi wa shule pia zitasaidia kuondosha msongamano wa wanafunzi madarasani sambamba na kuondosha wanafunzi kuingia shule nyakati za asubuhi na jioni.

Alisema mipango ya serikali iliyopo sasa pia ni ujenzi wa shule mpya ya sekondari huko katika eneo la kifundi Mkoa wa Kaskazini Pemba ili kusaidia kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi katika baadhi ya shule zilizopo maeneo mbalimbali ya Pemba.



Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali, akijibu hoja za wajumbe waliochangia bajeti ya wizara yake, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bil. 16/- zatengwa ukarabati nyumba za maendeleo visiwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi imetenga Sh. bilioni 16 kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati nyumba za maendeleo zilizoko Unguja na Pemba ambazo ziko katika hali mbaya na kutishia maisha ya wananchi.

Waziri wa wizara hiyo, Rahma Kassim Ali, alisema hayo jana wakati akifanya majumuisho na kujibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliotaka kujua mikakati ya wizara katika kuzihami nyumba za maendeleo zikiwamo za Michenzani ambazo baadhi tayari zimekimbiwa na wakazi kutokana na hali mbaya.

Rahma alisema serikali imetenga fedha hizo kwa kufahamu mazingira ya nyumba za maendeleo ambazo nyingi zilijengwa katika miaka ya 1960 wakati wa uongozi wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Shekhe Abeid Amani Karume.

Alizitaja nyumba zilizoko Kengeja, Pemba kuwa serikali imewataka wakazi wake kuondoka kutokana na uchakavu mkubwa na kuibuka kwa nyufa kubwa zinazotishia maisha ya wakazi wake.

Pia alisema nyumba za Mtemani, Pemba, pia zinakabiliwa na hali mbaya kutokana na kutofanyiwa matengenezo tangu zilipojengwa.

"Mheshimiwa Spika ni kweli nyumba nyingi za maendeleo zilizojengwa katika kipindi cha uongozi wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Shekhe Abeid Amani Karume, ziko katika hali mbaya. Tumeanza kuzifanyia matengenezo nyumba za Madungu, Chake Chake na baadaye kazi hiyo itaendelea hatua kwa hatua," alisema.

Pia alisema Shirika la Nyumba linakusudia kutekeleza mradi mkubwa wa nyumba za maendeleo nafuu katika maeneo ya Chumbuni Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

"Mheshimiwa Spika nataka niwape habari njema wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Shirika la Nyumba linatarajia kujenga nyumba kwa ajili ya makazi ya wananchi katika eneo la Chumbuni mkoa wa Mjini Magharibi," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23, walisema bado Shirika la Nyumba la Zanzibar halijaonyesha ubunifu katika utekelezaji wa majukumu yake katika kujenga nyumba za makazi zenye unafuu kwa wananchi.

Mwakilishi wa Chwaka, Issa Haji Gavu, alisema shirika hilo tangu lilipoanzishwa miaka saba iliyopita limeshindwa kuzifanyia ukarabati nyumba za maendeleo za Michenzani ikiwamo kuzipaka rangi kwa ajili ya kuleta haiba nzuri ya mji.

Naye Mwakilishi wa Mwera, Mihayo Juma Nhunga, alisema hajaridhishwa na utendaji wa Shirika la Nyumba la Zanzibar ambalo tangu liliponzishwa halijajenga nyumba za makazi kwa wananchi wala biashara.

Alimtaka Waziri kulijengea uwezo shirika hilo ikiwamo kulipa mtaji kwa ajili ya kujenga nyumba za makazi na biashara ili lijiongezee mapato.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI

INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,

DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**DAINESS E. MMARY** ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S1335/0005.** KILICHOTOLEWA NAWIZARA YA ELIMU MWAKA 2013 KUPITIA SHULE YA SEKONDARI KINDIKATI ILIYOPO KILIMANJARO WILAYA YA MOSHI VIJIJINI. ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA POLISI- DSM/PH**Q/RB/364738/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FELIX THOMAS CHUWA** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 447 ATU – NISSAN CARRAN.** Chassis namba **CRGE24072333.** Engine namba **TD273633858.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/218141/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**

**Shauri a madai/Ndoa Na 95/2022**

**Jina la Mdai: JOHN MBUNI**

**Jina la Mdaiwa: DEOGRATIAS MWANDAMI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: DEOGRATIAS MWANDAMI**
**WA KATORO-0757259988**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake Unaamriwa na Jamhuri uhudhurie Mahakamani ili ujibu madai ya Tsh. 3,900,000/-**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 6 Mwezi 6 Mwaka 2022 saa 2.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo..

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 26 Mwezi 5 Mwaka 2022

HAKIMU
PRIMARY COURT MAGISTRATE
GEITA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI Mkoa Wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......24 /2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SALUM KHALFAN AHMED WA SABASABA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AZIZA SALUM KHALFAN**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 07 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 23 Mwezi 05 Mwaka 2021

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NAMBA 95 YA MWAKA 2022**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU JOYCE DOROTH NAMPESYA**

**CECYLIA YUSUPH MASHAKA..................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 mwezi wa 6, 2022.

Imesainiwa Dar es Salaam, leo tarehe 17 mwezi wa 05, 2022.

NAIBU MSAJILI


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## OPEC wajadili kuongeza uzalishaji wa mafuta

**VIENNA,** AUSTRIA

NCHI wanachama wa shirika la wauzaji mafuta, OPEC zinajadiliana juu ya kuongeza uzalishaji wa mafuta muda mfupi baada ya Umoja wa Ulaya kupiga marufuku kuagiza nishati hiyo kutoka Russia.

Nchi za OPEC zinazoongozwa na Saudi Arabia na Russia zilipunguza utoaji wa mafuta kwa kiwango kikubwa mnamo mwaka 2020 kutokana na kupungua kwa mahitaji kulikosababishwa na janga la corona.

Mazungumzo kwa njia ya video yalianza jana alasiri kwenye makao makuu ya shirika hilo, mjini Vienna.

Nchi hizo zinatarajiwa kuongeza mafuta hadi mapipa 432,000 kila siku, utakapofika mwezi Julai.

Viongozi wa Umoja wa Ulaya walikubaliana mapema wiki hii kupiga marufuku theluthi mbili ya mafuta yanayoagizwa kutoka Russia kama duru ya sita ya vikwazo dhidi ya nchi hiyo kutokana na uvamizi wake nchini Ukraine.




## Marekani yamteua Hammer kuwa mjumbe maalum katika eneo la Pembe ya Afrika

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imetangaza kuwa balozi Mike Hammer ndiye atakayehudumu kama mjumbe maalum wa nchi hiyo katika eneo la Pembe ya Afrika.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alisema katika taarifa yake kwamba mjumbe huyo anachukua nafasi hiyo wakati ambapo eneo hilo linakabiliwa na misukosuko ya kisiasa. Blinken alisema mjumbe wa awali, David Satterfield, anajiandaa kuacha wadhifa wake huo.

Mjumbe mpya Mike Hammer atakabiliana na mzozo wa nchini Ethiopia na Sudan baada ya mapinduzi ya mwezi Oktoba.

# Russia yatangaza majaribio nyuklia

**MOSCOW,** RUSSIA

WIZARA ya Ulinzi ya Russia imetangaza kuanza mazoezi ya kijeshi ya kile kinachoitwa Kikosi cha Makombora cha Kimkakati ambacho kinamiliki nyuklia.

Mazoezi hayo yanahusisha makombora ya balestiki ya Yars, ambayo ni kizazi kipya cha kombora kilichojaribiwa kwa mara ya kwanza mnamo 2007.

Jeshi la Russia lilisema kuwa mazoezi hayo yanafanyika katika Mkoa wa Ivanovo karibu na jiji la Moscow na kuhusisha wafanyakazi 1,000 na magari zaidi ya 100.

Katika luteka hiyo, makombora hayatarushwa lakini yatajumuisha doria, kuweka mifumo ya makombora na kuwalinda kutokana na mashambulizi.

Mazoezi hayo yalitangazwa saa kadhaa baada ya Marekani kusema kuwa itawapa Waukraine mifumo ya hali ya juu ya roketi, ingawa taarifa ya jeshi la Russia iliyotolewa kwa vyombo vya habari haikuzungumzia taarifa kutoka Marekani.

**RUSSIA YADAI KUDUNGUA NDEGE YA UKRAINE**

Wizara ya ulinzi ya Russia ilisema kuwa ndege yake ya kikosi cha anga imeitungua ndege ya kivita ya Ukraine aina ya Sukhoi SU-25 katika jimbo la Mykolaiv.

Kulingana na taarifa iliyotumwa kwenye mtandao wa Telegram, Wizara hiyo pia imedai kutumia kombora kutoka kwa ndege aina ya precision air kupiga maeneo 21 nchini Ukraine.

Russia inadai imewauwa Wanajeshi 240 wa Ukraine na kuharibu zana 39 za kijeshi za nchi hiyo.

**RUSSIA YADHIBITI SEVERODONETSK**

Wizara ya Ulinzi ya Uingereza ilisema katika tathmini yake ya hivi karibuni kuwa Russia imechukua na kudhibiti sehemu kubwa ya Severodonetsk, mji ulio mashariki mwa Ukraine.

Taarifa hiyo ilieleza kwamba barabara kuu inayoingia kwenye eneo la Severodonetsk, huenda ikasalia chini ya udhibiti wa Ukraine lakini Russia inaendelea kupata mafanikio.

Hata hivyo, katika taarifa hiyo ilisema vikosi vya Russia vimepata hasara katika mchakato huo.

Tathmini hiyo inaongeza kuwa kuvuka mto wa Siverskyi Donets ambao ni kizuizi cha asili kwa vikosi vya Russia, ni muhimu wakati wanalinda eneo la Luhansk na kujiandaa kubadili mwelekeo hadi mkoa wa Donetsk.

Maofisa wa Ukraine wamekiri kwamba kiasi cha asilimia 80 ya Severodonetsk sasa iko mikononi mwa Russia, huku mapigano makali yakiendelea kwenye mitaa.



Severodonetsk, na mji mwingine pacha wa Lysychansk kwa wiki kadhaa umekuwa chini ya mashambulizi makubwa ya Russia.

**DENMARK KUJIUNGA ULINZI WA PAMOJA**

VIONGOZI wa Umoja wa Ulaya, wamesema uamuzi wa Denmark wa kujiunga na sera ya ulinzi wa pamoja ya umoja huo ni hatua ya kihistoria.

Kura ya maoni iliyopigwa nchini Denmark, imeashiria kwamba idadi kubwa ya wananchi wa nchi hiyo wanaunga mkono kuingia katika jumuiya hiyo.

Rais wa Halmashauri ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen na rais wa baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel, walisema uamuzi wa Denmark unatoa ujumbe wa nguvu wa kujizatiti juu ya ulinzi wa pamoja barani humo. Katika kura ya maoni, asilimia 67 ya watu wa Denmark waliunga mkono uamuzi wa nchi yao kujiunga baada ya kujiweka nje kwa muda wa miaka 30.

Waziri Mkuu wa Denmark Mette Frederiksen amesema matokeo hayo yametoa ujumbe muhimu kwa washirika wake wa Ulaya na Jumuiya ya Nato.

Kura hiyo ya maoni imefanyika nchini humo wiki chache, baada ya nchi jirani za Finland na Sweden kutoa maombi ya kujiunga NATO.



Baadhi ya makombora ya nyuklia ambayo Russia imetangaza kuanza kuyafanyia mazoezi. Hapa ilikuwa yakipitishwa mbele ya hadhara katika maadhimisho ya ushindi yaliyofanyika hivi karibuni. **PICHA: BBC**

# Marekani yaomba diplomasia mgogoro wa DRC, Rwanda

**KINSHASA,** DRC

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, ametoa wito wa kutatuliwa kwa njia ya kidiplomasia kwa mvutano unaoendelea kati ya nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Rwanda.

Blinken alisema hayo wakati akiwa kwenye ziara nchini DRC, kuwa Marekani inataka kuunga mkono amani na usalama na utulivu mashariki mwa DRC.

"Tunataka kuunga mkono sana juhudi muhimu za Kiafrika zinazoendelea," alisema.

Blinken alipongeza mazungumzo ya kuleta amani yaliyofanyika nchini Kenya kati ya serikali ya DRC na makundi ya waasi.

Kwa upande mwingine, Rais wa Angola Joao Lourenco, pia amefanya upatanishi na kueleza kwamba DRC imekubali kuwaachilia huru wanajeshi wawili wa Rwanda ambao wamezuiliwa.

Uhusiano kati ya nchi hizo mbili umedorora tangu kuwasili kwa Wahutu wa Rwanda mashariki mwa DRC wanaotuhumiwa kuwaua Watutsi wakati wa mauaji ya kimbari ya 1994.

**Habari zote BBC na DW**

## HABARI MICHEZO



Mwanamuziki wa bongofleva, Ali Kiba, akitumbuiza wakati wa uzinduzi wa mpango wa Marekani wa upatikanaji wa chanjo ya Global Vax, jijini Dar es Salaam jana. PICHA: JUMANNE JUMA

# YANGA, SIMBA ZAUNGANA KWENYE NANI ZAIDI

**Saada Akida na Shuffa Lyimo**

BAADA ya ubishani wa dakika 90, sasa Simba na Yanga zitaungana kuwa kitu kimoja kuhakikisha wanapambana kuleta maendeleo ya klabu hizo katika miundombinu kupitia kampeni ya Nani Zaidi kwa mashabiki kuchangua timu.

Kampeni hiyo inasimamiwa na Azam Media kwa ajili ya kuchangisha fedha kupitia mitandao ya simu na fedha hizo kupelekwa katika ujezi wa miundombinu ya ujenzi wa viwanja na hosteli za timu hizo.

Wakizungumza jana katika uzinduzi wa kampeni hiyo katika Hotel ya Serena, viongozi wa timu hizo, Simba ikiwakilishwa na Mtendaji Mkuu Barbara Gonzales na Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, huku Yanga ikiwakilishwa na Senzo Mazingiza na msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara, walisema wanaungana kwa ajili ya maendeleo.

Barbara alisema kampeni hiyo itakuwa kwa ajili ya kuhamasisha mashabiki na wanachama kuchangia klabu zao kwa ajili ya kutoka zilipo hasa katika suala la miundombinu ikiwamo uwanja na hosteli.

"Tumeingia katika michuano ya kimataifa na tulikaa na Azam, pamoja na wizara husika kwa ajili ya kuangalia njia ya kuboresha vipato vya klabu zote na hilo tumefanikiwa kwa kuandaa kampeni hiyo," alisema na aliongeza;

"Simba ina malengo ya kujenga uwanja katika kampeni hii tunaweka upinzani wetu pembeni na kuwa pamoja katika masuala ya maendeleo ya klabu hizi, tumekutana na viongozi wa Yanga kuangalia mchakato huu wa Nani Zaidi kati ya Simba na Yanga," alisema Barbara.

Alisema kwa Simba mchakato huo ni mara ya pili kwa kuwa walianza na (Tunaweza) na sasa wanaenda na kampeni hiyo ya nani zaidi ili kuweka kujiwezesha bila ya kukodi viwanja na hostel za kulala wachezaji.

"Baada ya mwisho wa msimu tunaweka wazi juu ya mipango yetu hasa katika harakati za ujezi wetu wa uwanja. Ni aibu kwetu kwa Simba na Yanga kukosa miundombinu ukiangalia timu za wenzetu kama ilivyo kwa Afrika Kusini, wamekuwa na miundombinu yao," alisema Barbara.

Alisema kwa kampeni hiyo Simba watapeleka fedha hizo moja kwa moja katika ujezi wao wa uwanja na miundombinu ya klabu hiyo na kuachana na utegemezi.

"Ukubwa wa klabu hizi sio kuchukuwa makombe, kufanya usajili wa wachezaji, bali kazi kubwa ni kuhakikisha tunakuwa na miundombinu bora zaidi, pia kutoa aibu kwa Taifa hasa zinapokuja klabu kutoka mataifa mengine wanapokuja kutembelea hizi klabu ambazo hakuna miundombinu ya kuwafanya wageni wetu kuwatembeza," alisema Barbara.

Naye Ahmed alisema jambo hilo ni kwa ajili ya maendeleo ya klabu hizo kwa mashabiki kuachana kupiga kelele za sasa kuwekeza na kutunishana misuri katika fedha.

Alisema kwa sasa timu zingine hazina cha kujifunza kupitia klabu hizo kingwe kwa sababu Simba na Yanga hakuna maendeleo yoyote aliyoyafanya hasa katika miundombinu.

"Ushindani na ubishi wetu unaishi dakika 90, lakini suala la maendeleo ya kila klabu lazima tuwe kitu kimoja na kuzungumza lugha moja, sasa hivi tunahitaji kufanya maendeleo makubwa," alisema.

"Ukiangalia Simba kwa mwaka mmoja tunakodi katika hosteli zaidi ya milioni 200, endapo tutakapokuwa na miundombinu yetu ikiwamo uwanja na hosteli kuna gharama zingine zinapungua na fedha hizo kufanya mambo mengine," alisema Ahmed Ally. Alisema katika kampeni yao ya kwanza ya (Tunaweza) walifanikiwa kuchangisha milioni 60, ambayo haitoshi katika ujezi huo wa uwanja na miundombinu mingine, lakini kampeni ya Nani Zaidi itasaidia kufikia malengo yao.

"Azam na wabia wetu watasaidia katika kampeni hii huku viongozi wanaendelea kufanya majukumu mengine ikiwamo usajili wa wachezaji na kutafuta kocha mpya."

"Ni aibu sana kuona Simba inakodi kila kitu, mashabiki wa Simba kujitokeza kuchangia kupitia kampeni hii ya Nani Zaidi, hatutarudi nyuma, fedha hizi tunaenda kujenga uwanja na miundombinu, na sio kula au kulipa mishahara," alisema Ahmed.

Kwa upande wa Yanga, Senzo alisema amefurahishwa na kampeni hiyo kwani itasaidia kuziinua kiuchumi klabu za Simba na Yanga, kupitia kura zitakazopigwa na mashabiki wa klabu hizo.

Alisema fedha zitapatikana kutokana katika kampeni hiyo zitapelekwa kwenye maendeleo mengine yamewekwa katika klabu hiyo ikiwamo miundombinu.

"Tunashukuru kuanzishwa kwa kampeni hii ya Nani Zaidi ni kampeni ambayo itasaidia kukuza klabu zetu hapa nchini na kulifanya soka letu lizidi kukua," alisema Senzo.

Alisema anaomba mashabiki wa Yanga wajitahidi kupiga kura na mchakato huo kufanyika wazi kwa kurushwa moja kwa moja kupitia kituo cha televisheni cha Azam.

Alisema wakati huu ni viongozi wa Simba na Yanga kukaa na kuzungumza lugha moja ya jinsi gani wataendeleza soka la Tanzania hasa kuwapo kwa miundombinu ya klabu hizo mbili kuna na mali yake.

Alisema kupitia kampeni ya Nani Zaidi kila mshabiki ataona idadi ya fedha ambazo zitakuwa zimekusanywa kwa muda wa wiki nzima.

Naye msemaji mkuu wa klabu hiyo, Haji Manara alisema amelipokea jambo hilo kwa mikono miwili na kuomba mashabiki wao wajitahidi kupiga kura ili klabu yao izidi kuwa bora.

"Kwa upande wa Yanga fedha ambazo zitapatikana kutokana na kura zitakazopigwa na mashabiki wetu moja kwa moja tutazipeleka kwenye mradi wa klabu yetu," alisema Manara.

Alisema mpaka sasa Yanga ni klabu pekee ambayo imefanikiwa kusajili wanachama 40,000 ambao tayari wamechukua fomu za kujiunga na klabu hiyo.

Alisema ni wakati wa klabu za Simba na Yanga kukaa pamoja kuzungumza jinsi gani ya kuboresha klabu hizo ili ziwe na hadhi ya juu.

## Mbeya City yaiwekea kambi Simba SC

**Na Saada Akida**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kutisha mechi za kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), timu ya Mbeya City inaingia kambini kwa ajili ya kujifua kwa mchezo wao dhidi ya Simba utakaopigwa Juni 16, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule alisema baada ya mapumziko mafupi leo wanatarajia kurejea kambini kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Simba.

"Hatukuwa na matokeo mazuri katika michezo yetu ya mwisho na kupoteza hapa nyumbani dhidi ya Coastal Union, sasa tunarejea uwanjani kufanyia kazi mapungufu yetu kwa ajili ya mchezo wetu ujao dhidi ya Simba," alisema Lule.

Alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu mechi ya kwanza walipata matokeo mazuri katika uwanja wa kwao na sasa wanahitaj kujiandaa vizuri kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wao wa ugenini.

Kocha huyo alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa kwa sababu uchache wa pointi ambazo wanapishana kwa timu za chini na timu inapopoteza mchezo mmoja inashuka hadi nafasi ya chini na anayeshinda kupanda juu.

## Waziri awapongeza wasanii kwa ubunifu

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, amewapongeza wasanii kwa kuwa wabunifu wa kuzalisha filamu zenye viwango vya kimataifa.

Mchengerwa alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akizindua filamu ya Vita N'kuvute iliyozalishwa na Kijiweni Production ambayo itaonyeshwa kwenye matamasha na nyumba za sinema.

Alisema kazi iliyofanyika kubwa na nzuri, inayoweza kushindanishwa kimataifa na kwamba ni filamu ambayo ina ubunifu mkubwa na uhalisia tofauti na nyingine.

Aliahidi kuwa serikali chini ya wizara yake, itaendelea kuunga mkono filamu za Watanzania na wasanii wenyewe na kwamba fedha zimetengwa za kutosha za kusimamia utekelezaji wake.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Kijiweni Production, Amil Shivji, alisema filamu hiyo wameshirikiana na BigWorld Cinema (SA) na Nico Filamu (DE) katika kuiandaa.

Akizungumzia filamu hiyo alisema ni hadithi ya mapenzi na siasa katika miaka ya mwishoni ya Zanzibar chini ha Ukoloni wa Waingereza.

"Filamu hii imeonyesha tamaduni ya Pwani za miaka za 50 katika mgawanyo wa kitabaka na ubaguzi wa rangi ambao uliwekwa na utawala wa kikoloni," alisema Shivji.

## ZISIKUPITE

### SALAH KUONDOKA
MSHAMBULIAJI wa Liverpool kutoka Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29, angependelea kujiunga na timu pinzani ya Ligi Kuu msimu ujao ikiwa hakuna mkataba mpya wa kusalia kwa wekundu hao. ***(The Athletic)***

### MANE NAE
MSHAMBULIAJI wa Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30 anataka kuondoka Liverpool msimu huu wa joto, huku klabu ya Bayern Munich ikiwa na ushindani mkubwa katika kuiwania saini yake. . ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### KOUNDE ATAKIWA
CHELSEA wameanza mazungumzo na Sevilla kuhusu kumsajili beki wa Ufaransa mwenye thamani ya pauni milioni 50, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 23, ambaye aliisaidia klabu hiyo ya Hispania kushinda Ligi ya Europa mwaka 2020. ***(Sport)***

### EKITIKE AJADILIWA
KLABU ya Newcastle ipo kwenye majadiliano juu ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Reims mwenye umri wa miaka 19, Mfaransa Hugo Ekitike katika mkataba wa pauni milioni 25 pamoja na zaidi. ***(Daily Mail's Craig Hope, Twitter)***

### DE JONG NA MAN
BAADA ya kutangaza kuachana na Paul Pogba na Jesse Lingard, Manchester United imeanza mazungumzo na Barcelona kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, kuhusu uhamisho wa pauni milioni 72.5 kwenda Old Trafford. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### SAVIC AWANIWA
KLABU ya Manchester United inataka kumnunua kiungo wa kati wa Lazio na Serbia, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 27, kama mbadala wa Frenkie De Jong. ***(GiveMeSport)***

### POGBA KURUDI JUVE
KLABU ya Juventus ina imani kwamba wamekubali mpango wa kumrejesha Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, wakati mkataba wa kiungo huyo wa kati wa Ufaransa na Manchester United utakapokamilika mwisho wa mwezi huu. ***(90min)***

### KEITA KUBAKI
LIVERPOOL wanapanga kumpa kiungo wa Guinea, Naby Keita mwenye umri wa miaka 27 mkataba mpya. Paris St-Germain wanamtaka mchezaji huyo, lakini Wekundu hao wanatumaini Keita atabakia hadi msimu ujao wa joto wakati mkataba wake wa sasa utakapomalizika. ***(The Athletic)***

### PALHINHA HUYO WOLVES
KLABU ya Wolves inakaribia kumsajili Joao Palhinha wa Sporting Lisbon, huku kiungo huyo wa kati wa Ureno mwenye umri wa miaka 26, akikubali kujiunga kwa mkataba wa muda mrefu kwa ada ya takriban pauni milioni 20. ***(Sun)***

### PHILLIPS ATAKIWA
MANCHESTER City wanamtaka kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26, lakini Leeds United bado wana matumaini ya kumbakisha mchezaji huyo. ***(Sun)***

### BELLINGHAM AWINDWA
KLABU ya Real Madrid inamtaka kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, lakini hawatamnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 hadi mwaka 2023. ***(Bild)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LUKAKU YUKO TAYARI KUKATWA MSHAHARA

## Ni ili arudi Inter Milan kuliko kuendelea kucheza pale Chelsea na sababu kubwa ni...

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Romelu Lukaku yuko tayari kukatwa mshahara mkubwa ili kurejea Inter Milan msimu huu wa joto, kwa mujibu wa BBC Sport.

Lukaku alistahimili msimu mbaya sana Stamford Bridge baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 97.5 kutoka Inter majira ya joto yaliyopita.

Ingawa alianza kampeni vizuri, mahojiano ambayo sasa ni mashuhuri na vyombo vya habari vya Italia - ambapo alikiri alitaka kuichezea tena Nerazzurri .

Inter sasa wamethibitisha nia yao ya kumrejesha raia huyo wa Ubelgiji pale San Siro, na Chelsea haitamzuia mchezaji huyo iwapo atashinikiza kuhama.

Lukaku ana nia ya kufanikisha mpango huo, na kwa mujibu wa Daily Mail, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 yuko tayari kupunguza mshahara wake ili kurejea Italia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Inter, Beppe Marotta amekiri nia ya klabu hiyo kutaka kumnunua tena Romelu Lukaku - na Chelsea haitamzuia mchezaji huyo.

Inasemekana kuwa Inter wanaamini kuwa fowadi huyo angefurahi kurudi nchini humo kwa mshahara aliokuwa nao kabla ya kuondoka Chelsea mwaka jana - karibu pauni 125,000 kwa wiki, ambayo itajumuisha punguzo la takribani pauni milioni 3 kwa mwaka kwenye mapato yake ya sasa pale Stamford Bridge.

Nerazzurri wanataka kushirikiana na Lukaku na Paulo Dybala, ambaye ataondoka Juventus baada ya kumalizika kwa mkataba wake, ingawa watahitajika kumuuza Lautaro Martinez.

Akizungumzia nia ya Inter kwa wachezaji wote wawili siku ya Jumatatu, Mkurugenzi Mtendaji wa Inter Marotta alikiri kwamba mipango iko mbioni.

"Hakuna haraka kwa upande wetu, hatuwezi kuharakisha," alisema. "Hakika tayari tumeanza kuweka msingi."

"Inahitaji ubunifu na ujasiri kufanya hatua fulani. Ni wazi kuwa msingi wa timu utabaki. Sisi ni Inter na kwa hivyo tunataka kila wakati kufikia malengo makubwa."


BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,001,6

MECHI KALI
FRANCE
VERSUS
DENMARK
1 | 1.67
X | 3.70
2 | 4.96

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POGBA RASMI KUONDOKA MAN UNITED



**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba ataondoka Manchester United kwa uhamisho huru, mkataba wake utakapokwisha mwishoni mwa mwezi huu, klabu hiyo imethibitisha.

Pogba mwenye umri wa miaka 29, alivunja rekodi ya dunia kwa dau la pauni milioni 89 alipojiunga tena na klabu hiyo akitokea Juventus mwaka 2016.

Alicheza mechi 27 katika msimu wa mwisho wa majeruhi katika kipindi chake cha pili.

"Ulikuwa mwisho wenye utulivu kwa United ambao ulileta nyakati nyingi nzuri kwa kila mtu," klabu ya Old Trafford ilisema katika taarifa.

"Kwa kijana aliyejiunga na akademi akiwa na umri wa miaka 16 na kucheza zaidi ya mechi 200 za United na kubeba Kombe la Vijana, pamoja na mataji mawili ya ubingwa ni jambo linalopaswa kupongezwa na kushangiliwa."

Pogba alijiunga na United kwa mara ya kwanza akitokea klabu ya Le Havre ya Ufaransa mwaka 2009 akiwa na umri wa miaka 16 na alikuwa sehemu ya timu ya vijana iliyoshinda Kombe la Vijana mwaka 2011.

Alicheza mechi saba pekee za wakubwa kabla ya mkataba wake kuisha Julai 2012 na akaondoka na kujiunga na Juventus.

Pogba alishinda tuzo nane mjini Turin, ikiwa ni pamoja na mataji manne mfululizo ya Serie A, kabla ya kurejea tena Old Trafford.

Alishinda Kombe la EFL na Ligi ya Europa katika msimu wake wa kwanza katika klabu hiyo.

Kutoelewana na aliyekuwa kocha wa wakati huo Jose Mourinho kulimfanya apoteze unahodha mwaka 2018 na majeraha yaliyoathiri uchezaji wake.

# Dybala: Nina furaha Italia

**LONDON, England**

PAULO Dybala amefichua kuwa ana furaha kucheza nchini Italia, ingawa amekiri kwamba angependa kucheza ligi nyingine kabla ya kustaafu kucheza soka.

Dybala anaondoka Juventus msimu huu wa joto kwa uhamisho wa bure baada ya miaka saba katika klabu hiyo na kwa sasa anaonekana uwezekano wa kusalia Serie A na Inter.

Kama ilivyoripotiwa mwezi uliopita na 90min, Inter iliibuka kama kivutio zaidi kwa saini yake ilipobainika kuwa angeondoka Turin.

Fowadi huyo aliulizwa kuhusu mustakabali wake baada ya Fainali kuyisaidia Argentina kuifunga Italia 3-0 juzi Jumatano, alifichua kwamba, alikuwa na furaha zaidi kubakia Serie A zaidi ya msimu huu wa joto.

"Nimetulia kabisa, watu wanaofanya kazi nao wanajali. Ninajitolea kucheza. Nchini Italia nina raha sana, wananichukulia kama Muitaliano. Lakini bado ningependa kujua ligi zingine," aliiambia ESPN Argentina. .

Inter wanaendelea kufanyia kazi mpango wa kumsajili Dybala huku makamu wa rais Javier Zanetti akiwakejeli mashabiki kuhusu matarajio yake ya kucheza mbele na mwenzake Lautaro Martinez msimu ujao.

"Labda. Soko la uhamisho linafunguliwa, tuna muda mwingi - sisi ni klabu ambayo lazima itumie fursa, ikiwa hivyo ndivyo tutakavyotathmini," aliiambia Sempreinter.

"Lazima pia tuwe wakweli, vikwazo tunavyokabiliana navyo unavijua, lakini tunazungumza kuhusu mchezaji bora linapokuja suala la Dybala."

## HABARI MICHEZO

# 641,108/-

# UNAVYOWEZA KUSHINDA SUPA JACKPOT 5 KWA MPIGO

**Na Dennis Fussi**

KAMA ulikuwa hujasikia ama umesikia lakini hujaelewa vizuri Sportpesa wiki iliyoisha walizindua Jackpot mpya inayokwenda kwa jina la Supa Jackpot.

Jackpot hii inahusisha timu 17 ambapo zawadi kubwa kabisa ni kuanzia bilioni moja kama utakuwa umeshinda mechi zote zilizowekwa kwa wikiendi hiyo.

Kipengele namba moja ni cha timu 17 ambacho ukishinda unaondoka na kuanzia bilioni moja kutegemeana na Jackpot imesimamia kiasi gani. Kipengele hiki bonasi zake zinaanzia timu 16 hadi 13.

Kundi la pili au kipengele namba mbili ni cha timu 16 ambacho ukipatia mechi zote unashinda kuanzia Tsh milioni 750. Kipengele hiki bonasi zake zinaanzia timu 15 mpaka mechi 11.

Kundi la tatu au kipengele namba tatu ni cha timu 15 ambacho ukipatia mechi zote kwa usahihi unashinda kuanzia Tshs milioni 500. Kipengele hiki bonasi zake zinaanzia mechi 14 mpaka mechi 10.

Kipengele cha nne cha Supa Jackpot ni cha timu 14 ambacho ukipatia mechi zote kwa usahihi utashinda kuanzia Tsh milioni 300. Kipengele hiki bonasi zake zinaanzia timu 13 mpaka timu 10

Na kipengele cha mwisho hiki ni kipengele ambacho kimezoeleka kila siku ni cha timu 13 ambacho ukipatia kwa usahihi unashinda kuanzia Tsh mil 200.

Cha ziada ambacho ni mabadiliko kidogo ni kwenye kombinesheni. Kama mtakumbuka Jackpot iliyoliwa ilikuwa unaweza kucheza dabo kombinesheni saba. Kwenye hii Jackpot mpya una uwezo wa kucheza dabo kombinesheni 10.

Kwa muktadha huu mchezaji wa Supa Jackpot ana uhuru wa kucheza jackpot zote tano na kama atapatia ubashiri wake kwa usahihi basi anashinda Jackpot zote au bonasi zote.

Cha mwisho kumalizia kwa sasa Sportpesa imekupa fursa ya kucheza bila bando kwa watumiaji wa Vodacom, Tigo na Airtel ambapo kwa wachezaji wenye simu janja au (smart phone) na wanaotumia huduma ya simu za vitochi au maarufu viswaswadu kwa menyu yetu ya *150* 87# wanacheza bure bila malipo yoyote.

Akiongelea huduma hii meneja uhusiano na mawasiliano wa Sportpesa Sabrina Msuya aliwataka watanzania kuchukua fursa hiyo kwani inawarahisishia katika uchezaji wao.

''Kwenye eneo hili si watumiaji wa simu janja tu ama Smartphones ambao watanufaika. Kuna wachezaji wetu wanaotumia menyu ya *150* 87# ambao si wengine bali wale wenye simu za vitochi almaarufu kama viswaswadu nao watafurahia.

''Niwaombe watanzania mchukue fursa hii ya kucheza bila bando kwani inawapa urahisi wa kutumia huduma zetu kwa urahisi.''.

Kucheza na Sportpesa piga *150*87# kujisajili, au tembelea www.sportesa.co.tz

# Stars yapaa Benin na matumaini kibao

**Na Adam Fungamwango**



KIKOSI cha timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars kilipaa jana kwenda nchini Benin kucheza mechi ya kwanza ya kundi F dhidi ya Niger, kusaka tiketi ya kucheza fainali ya Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023 zinazotarajiwa kuchezwa nchini Ivory Coast, huku meneja Nadir Haroub 'Cannavaro' akisema wana matumaini makubwa ya ushindi.

Mechi hiyo inatarajiwa kupigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa L'amitie jijini Cotonou nchini Benin, kwani timu hiyo haichezi nchini kwao Niger kutokana na viwanja vya huko kutokidhi vigezo vya Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Cannavaro amesema kuwa matumaini makubwa ya ushindi kwenye mechi hiyo yanatokana na kwamba wanakwenda kucheza kwenye uwanja ambao wameuzoea zaidi kuliko hata wapinzani wao.

Mara ya mwisho Stars kucheza kwenye uwanja huo ilikuwa ni Oktoba 10 mwaka jana, ilipocheza dhidi ya wenyeji Benin na kushinda bao 1-0 lililofungwa na Simom Msuva kwenye michuano ya kusaka tiketi ya kufuzu Kombe la Dunia litakalofanyika mwishoni mwa mwaka huu nchini Qatar.

"Ni uwanja ambao tunaujua na tumeuzoea, tumeshacheza dhidi ya wenyeji Benin kwa hiyo wachezaji wetu hawatopata shida," alisema meneja huyo.

Alisema matumaini mengine ya ushindi yanatokana na kwamba Stars huwa na matokeo mazuri inapocheza kwenye viwanja vya ugenini.

"Ukiangalia hata kwenye kinyang'anyiro cha kufuzu Kombe la Dunia, tulipata matokeo mazuri ugenini, sasa safari hii tunataka tuwe tunashinda ugenini na nyumbani pia. Tutapambana kupata matokeo mazuri na huu ni mwaka wetu," alisema nahodha huyo wa zamani wa timu hiyo.

Stars ipo kwenye Kundi F, pamoja na timu za Niger, Argeria, na Uganda.

Fainali za AFCON zinatarajiwa kuchezwa nchini Ivory Coast Juni 23, na Julai 23 mwakani.


# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII

## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/06/22 | 18:00 | Atletico Tucuman vs Colon de Santa Fe | 2.90 | 3.15 | 2.42 |
| 02. 04/06/22 | 19:00 | Finland vs Bosnia & Herzegovina | 2.60 | 3.05 | 2.70 |
| 03. 04/06/22 | 19:00 | Lithuania vs Luxembourg | 3.20 | 3.00 | 2.30 |
| 04. 04/06/22 | 21:45 | Montenegro vs Romania | 2.95 | 3.05 | 2.43 |
| 05. 04/06/22 | 21:45 | Italy vs Germany | 2.48 | 3.25 | 2.70 |
| 06. 05/06/22 | 01:00 | CA Patronato Parana vs Velez Sarsfield | 3.05 | 3.10 | 2.32 |
| 07. 05/06/22 | 01:00 | CA Platense vs CD Godoy Cruz | 2.95 | 3.25 | 2.31 |
| 08. 05/06/22 | 02:00 | Vancouver Whitecaps FC vs Real Salt Lake | 2.43 | 3.30 | 2.75 |
| 09. 05/06/22 | 02:30 | AC Goianiense GO vs SC Corinthians SP | 2.95 | 3.00 | 2.46 |
| 10. 05/06/22 | 08:00 | Renofa Yamaguchi vs Thespakusatsu | 2.55 | 3.05 | 2.80 |
| 11. 05/06/22 | 08:00 | Omiya Ardija vs Mito Hollyhock | 2.70 | 3.30 | 2.44 |
| 12. 05/06/22 | 08:00 | JEF United Ichihara Chiba vs Vegalta Sendai | 2.46 | 3.05 | 2.90 |
| 13. 05/06/22 | 08:00 | Blaublitz Akita vs Roasso Kumamoto | 2.85 | 3.00 | 2.50 |
| 14. 05/06/22 | 17:00 | EC Juventude RS vs Fluminense FC RJ | 2.80 | 3.00 | 2.60 |
| 15. 05/06/22 | 19:00 | Union de Santa Fe vs CA Tigre | 2.30 | 3.00 | 3.20 |
| 16. 05/06/22 | 21:45 | Kosovo vs Greece | 3.05 | 3.25 | 2.25 |
| 17. 05/06/22 | 22:00 | SE Palmeiras SP vs Atletico Mineiro MG | 2.28 | 3.20 | 3.05 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 03/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2894 | Shandong Luneng vs Hangzhou NG | 1.23 | 5.50 | 9.63 |
| 17:00 | 4624 | Kazakhstan vs Azerbaijan | 2.63 | 2.98 | 2.83 |
| 18:00 | 3165 | FA Siauliai B vs FK Minija | 1.71 | 3.94 | 3.84 |
| 18:00 | 4481 | FK Silas vs FK Panevezys B | 1.53 | 4.32 | 4.62 |
| 18:30 | 1528 | Japs vs Kerho 07 | 2.76 | 3.40 | 2.26 |
| 18:30 | 2477 | FC KTP vs Pif Jalkapallo | 1.40 | 4.43 | 6.30 |
| 18:30 | 3642 | KPV Kokkola vs FF Jaro | 3.44 | 3.39 | 1.95 |
| 18:45 | 1864 | CR Belouizdad vs MC Magra | 1.45 | 3.93 | 6.49 |
| 18:45 | 3473 | USM Alger vs Ol. Medea | 1.29 | 4.51 | 9.42 |
| 18:45 | 4552 | RC Relizane vs RC Arbaa | 5.32 | 3.89 | 1.53 |
| 19:00 | 2445 | SV 09 Arnstadt vs Erfurt | 23.51 | 11.75 | 1.03 |
| 19:00 | 3310 | Linkopings W vs Rosengard W | 4.21 | 3.62 | 1.70 |
| 19:00 | 4710 | Latvia vs Andorra | 1.49 | 3.88 | 7.05 |
| 19:00 | 4957 | Tromso IL 2 vs Senja FK | 1.19 | 6.49 | 9.44 |
| 19:15 | 4074 | Germany U21 vs Hungary U21 | 1.11 | 7.26 | 16.67 |
| 19:30 | 1126 | Middelfart vs Kolding IF | 2.95 | 3.54 | 2.09 |
| 19:30 | 1855 | FC Sydvest 05 vs Aarhus Fremad 2 | 2.95 | 3.94 | 1.97 |
| 19:30 | 3818 | KS Stolem Gniewino vs Sokol Kleczew | 3.78 | 3.48 | 1.82 |
| 19:30 | 5769 | BK Avarta vs Herstedoster IC | 1.55 | 4.33 | 4.43 |
| 19:45 | 4272 | Moldova U21 vs Netherlands U21 | 34.40 | 9.83 | 1.03 |
| 20:00 | 2473 | Holbaek vs Koge Nord FC | 1.37 | 4.91 | 6.09 |
| 20:00 | 4419 | Frederikssund vs Greve | 2.51 | 3.93 | 2.24 |
| 20:00 | 5358 | Goeppinger SV vs TSG Backnang | 2.22 | 4.24 | 2.42 |
| 20:00 | 5401 | BK Astrio vs Tolo IF | 1.46 | 4.81 | 4.81 |
| 20:00 | 5863 | FA 2000 vs Aarhus Fremad | 3.15 | 3.69 | 1.96 |
| 20:30 | 2575 | Kvarnsvedens IK vs Sandvikens AIK FK | 2.36 | 3.83 | 2.41 |
| 20:30 | 3379 | Express IL vs Uraedd FK | 2.33 | 4.02 | 2.36 |
| 21:00 | 3879 | Floresta CE vs Uniclinic CE | 1.64 | 3.19 | 5.69 |
| 21:30 | 4684 | Fjolnir vs KV Vesturbaer | 1.33 | 5.11 | 6.68 |
| 21:45 | 1169 | Belarus vs Slovakia | 5.83 | 3.57 | 1.62 |
| 21:45 | 2037 | France vs Denmark | 1.67 | 3.70 | 4.96 |
| 21:45 | 3887 | Croatia vs Austria | 2.11 | 3.24 | 3.49 |
| 21:45 | 3902 | Liechtenstein vs Moldova | 5.05 | 3.49 | 1.71 |
| 21:45 | 3958 | Belgium vs Netherlands | 2.23 | 3.43 | 3.03 |
| 22:15 | 1035 | Afturelding vs Grotta | 2.94 | 4.22 | 1.91 |
| 22:15 | 1277 | Kordrengir vs UMF Grindavik | 2.00 | 3.54 | 3.14 |
| 22:15 | 2849 | Ellidi vs Kari | 2.16 | 4.22 | 2.50 |
| 22:15 | 3315 | Volsungur vs KF Fjallabyggd | 1.50 | 4.80 | 4.90 |
| 22:15 | 3820 | Haukar vs Aegir | 2.27 | 3.94 | 2.46 |
| 22:15 | 3852 | KH Hlidarendi vs Vidir | 7.44 | 6.46 | 1.23 |
| 22:15 | 4120 | KFG vs IH Hafnarfjordur | 1.24 | 6.07 | 7.64 |
| 22:15 | 4434 | Augnablik vs Vaengir Jupiters | 2.11 | 3.79 | 2.75 |
| 23:00 | 1182 | Club Guarani vs Libertad Asuncion | 3.35 | 3.84 | 1.85 |
| 23:00 | 1748 | Cerro Porteno vs Resistencia FC | 1.06 | 9.86 | 19.72 |
| 23:00 | 3456 | Sportivo Ameliano vs Olimpia Asuncion | 5.67 | 5.48 | 1.35 |
| 23:00 | 3835 | Saint-Martin vs Aruba | 6.30 | 4.63 | 1.38 |
| 23:00 | 5867 | SOL De America vs 12 de Octubre de Itaugua | 1.52 | 4.05 | 5.13 |
| 23:30 | 1807 | Sint Maarten vs Virgin Islands | U.s. | 2.35 | 3.38 |
| 23:30 | 4370 | Turks And Caicos Islands vs Bonaire | 3.48 | 3.38 | 1.93 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Juni 3, 2022
Nipashe



**Lukaku yuko tayari kukatwa mshahara**



Msemaji wa Simba, Ahmed Ally (kushoto), akiwa pamoja CEO Barbara Gonzal (wapili kushoto), Senzo Mazingiza, Hajji Manara na Hassan Bumbuli (kulia). Habari Uk. 20. **PICHA: SAADA AKIDA**

# MAKOCHA KIBAO WAITAKA SIMBA

## ●●●Wajitokeza na kutuma maombi ya kuinoa klabu hiyo baada ya kumtimua Pablo...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema kuwa imepokea maombi kwa simu na barua pepe kutoka kwa mawakala na makocha mbalimbali duniani wakitaka kibarua cha kuifundisha timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao, baada ya kumtimua kocha wao Pablo Franco.

Pamoja na hayo, klabu hiyo imesema imekuwa ikiingia makubaliano na baadhi ya wachezaji, lakini haijaanza rasmi usajili hadi hapo itakapitia ripoti iliyoachwa na kocha aliyepita, lakini na mapendekezo ya kocha mpya atakayekuja.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema jana tangu ilipoachana na kocha Pablo na kutangaza rasmi Mei 31, imekuwa ikipata maombi kutoka kwa makocha mbalimbali kurithi mikoba yake.

"Kuna wakati kila baada ya saa moja tunapata simu pamoja na barua pepe, lakini tangu kocha aondoke tumepata maombi mengi kutoka kwa mawakala ambao wamekuwa wakituambia wana makocha wazuri, pia makocha wenyewe kutoka pande mbalimbali za dunia wamekuwa wakitupa wasifu wao ili tu kuisaka kazi ya kocha aliyepita. Kuminika kwa maombi haya siyo kwamba kuna uhaba wa ajira la hasha, ila ni kwa ajili ya ukubwa na Simba, kila kocha mkubwa na mwenye viwango angependa kuja kuifundisha Simba, lakini hiyo haitufanyi sisi tuingie kwenye presha hizo, tutakaa na kuangalia nani atatufaa. Hata sisi tunafuatilia mpira tunafahamu makocha wazuri, kwa hiyo atakayekidhi vigezo ndiyo atakayekuwa kocha wa Simba na tunawaahidi wanachama na mashabiki wa Simba tutawaletea kocha mwenye viwango vya dunia." Alisema.

Kuhusu usajili alisema harakati za kuingia makubaliano zimeanza, lakini hawajaanza usajili rasmi.

"Usajili hatujaanza rasmi, tumeelekeza jicho kusaka kocha, tukimpata kocha ndani ya wiki hizi mbili, ndiyo tutaanza mipango ya kukaa na kocha kutuambia anataka wachezaji wa aina gani na yeye aone wachezaji waliopo. Mapendekezo ya kocha aliyepita na kocha mpya ndiyo yatatuelekeza na kutupa mwanga na taswira ni aina gani ya wachezaji ambao tunakwenda kuwasajili." Alisema Ahmed.

# Mabadiliko kanuni Ligi Kuu yaanza

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania imeanza kupokea maoni ya maboresho ya kanuni za ligi kwa ajili ya msimu ujao.

Kwa mujibu wa mtandao rasmi wa Instagram na Shirikisho la Soka Nchini (TFF) na wa Bodi, wamewataka wadau wote wa soka kutuma maoni kuhusu maboresho ya kanuni ili kuifanya ligi kuwa bora zaidi.

Mdau anayetaka kutoa mapendekezo ya maoni yake, au maboresho anatakiwa kutuma kwa barua pepe 'maoni@ligikuu.co.tz.'

"Kanuni bora na rafiki huzaa ligi bora." ilimalizia taarifa hiyo ya Bodi ya Ligi.

Maoni hayo hupelekwa kwenye kamati husika kuchakatwa, kurekebishwa na hatimaye kupitishwa kwa ajili ya msimu husika.

**Wakati Ligi Kuu msimu huu ikiendelea, baadhi ya mashabikiwa soka, wakiwamo hata baa dhi ya viongozi wa klabu mbal imbali wamekuwa wakilalamika baadhi ya kanuni hasa pale zinapoanza kufanya kazi.**

Hata hivyo, ni hao hao baadhi ya viongozi wa klabu ambao nao wanahusika kuziunda na kuzipitisha, lakini zinapoanza kuwagusa wanalalamika.

Baadhi ya mashabiki wameonekana kulalamikia zaidi kanuni ya kuwafungia viongozi kwa miaka mitano au zaidi wakidai imepitwa na wakati, pia kanuni nyingine inayoonekana hawaipendi sana ni ile ya kuweka kikomo cha wachezaji wa kigeni mwisho wanane tu kwenye mchezo mmoja, wakati klabu zikiruhusiwa kusajili idadi ya wachezaji 12.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >